**Mchungaji na Elimu ya Kikristo**

Mchg. Dkt. Emmanuel Kileo

## 1. Utangulizi

Wapendwa wachungaji wenzangu,
Ni imani yangu kubwa kuwa mada ifuatayo "Mchungaji na Elimu ya Kikristo" katika mkutano huu mkubwa – Mkutano wa Wachungaji wote KKKT - ni mada muhimu hasa katika ulimwengu wetu unaobadilika.

Wachungaji na walimu wengine wa Elimu ya Kikristo wanakutana na maswali mapya kila siku katika mazingira yao.

Mara nyingi majibu yanayotolewa sasa hayakidhi au hayatoshelezi, hata kama ni kwa maswali yanayofanana na yale ambayo zamani yaliulizwa, na ndio sababu ya kukutana hivi wote ili, pamoja na kuonesha umoja wetu, lakini pia kubadilishana uzoefu katika changamoto mpya zilizojitokeza. Ni sawa na kusema, hakuna haja ya kujichimbia kwenye Dayosisi zetu au idara zetu za Elimu ya Kikristo, tukipambana kuvumbua "tairi" la Elimu ya Kikristo. Lilishagunduliwa! Inaendelea Kuboreshwa! Tuunganishe nguvu pamoja kuikamilisha!

Sasa kwenye mada niliyopewa imegusa kada moja tu katika kada nyingi za wafundishaji wa Elimu ya Kikristo. Katika Dayosisi nyingine kuna waalimu maalumu wa Elimu ya Kikristo, wamesoma theologia na ualimu, kuna wadiakonia, kuna wainjilisti, kuna wahudumu wa sharika (parish workers), kuna na wale wengine wa kujitolea. Hata hivyo, mada inamlenga Mchunagji zaidi maana Elimu ya Kikristo ni jambo linalomhusu kama wajibu wake mkuu, hata kama anaweza kukasimisha (delegate) wajibu huo kwa wengine.

Kutofanya Elimu ya Kikristo kuwa wajibu mkuu wa Mchungaji kuna changamoto zake, hapa natoa mifano ifuatayo:

- Mchungaji mmoja alipopita kwa bahati mbaya kwenye chumba ambacho watoto wa Shule ya Jumapili walikuwa wanaendesha ibada yao, mwalimu wao aliwaamrisha: "Amkieni". Watoto kama kawaida yao walitii na walisimama na kumsalimu Mchungaji wakisema kwa sauti: "Shikamoo Mungu!" Yawezekana huyu baba Mchungaji aliitikia pia "marahaba" maana hakusikia vizuri salamu ya watoto kwa haraka zake. Yeye unajua ni wa watu wazima, sio watoto – Mchungaji mmoja ametumia lugha kali kidogo akasema wachungaji wa namna hii wanashughulika na "mbwa wazee" (you can not teach them new tricks). Au yeye hasa anafanya utawala na uendeshaji wa usharika.
- Mtoto mwingine alipoulizwa alimwaona wapi Mchungaji wao wa Usharika alisema kwa uhuru kabisa: "Pale Kisimani" - maana Mchungaji pia alichota maji pale kisimani. Niliona uso wa Mchungaji umesinyaa mara moja.
- Mchungaji wa mazoezi mwenzetu alipoanza mazoezi yake baada ya muda alitamani kujua usharika ule ni mkubwa kiasi gani: Alikwenda kila upande. Alipokwenda akafika mahali akakutana na watoto na hawakuamkia "shikamoo Mchungaji" na sio "shikamoo Mungu" alijua sasa yupo usharika jirani. Na aliweza kurudi maana amefika mwisho wa usharika.

Elimu ya Kikristo siyo elimu ya watoto tu, ni elimu ya watu wazima pia. Nilipohubiria wazee kwenye moja ya nyumba za wazee, mmoja wao aliuliza kwa sauti katikati ya mahubiri akisema: "Jamani kuna mtu anaweza kuniambia huyu mhubiri wa leo anataka kutuambia nini…?" Hapa jambo jingine muhimu ilikuwa wazi kwangu: Elimu kwa wazee ni tofauti na elimu kwa watoto. Swali kubwa siyo kufundisha, lakini unafundishaje?

Mchungaji rafiki yangu aliniambia: Kwa wazee nenda na alama zinazoweza kuwakumbusha, maana wakati vijana wanaishi kwa matumaini, wazee huishi kwa kumbukumbu. Huhitaji kuwaambia wazee leo ni siku ya Bwana ya 9 kabla ya Pasaka – "Septuagesima". Hawataelewa. Siku ya Pasaka beba taji la miiba; Krismasi beba boksi la zawadi; Ujio wa Roho Mtakatifu beba njiwa, n.k. Hii ni kusema: Elimu ya Kikristo ni kwa marika yote na kila rika kwa namna yake.

Ni wazi kuwa kazi ya kufundisha Elimu ya Kikristo inamhusu Mchungaji. Yeye ndiye mtheologia mkuu wa usharika! Mchungaji ni msimamizi wa Mafundisho yote ya Kikristo Usharikani kwake. Ni msimamizi wa missioni - wito mkuu: "Enendeni ulimwenguni kote..."

Mchungaji anaonekana kama mfundishaji, Mchungaji kama mwezashaji, Mchungaji kama mtoa dira, Mchungaji kama mwandaaji, nk. Wachungaji wanaofahamu vizuri hili huandaa pamoja na watumishi wao mahubiri, zamani kulikuwa na siku maalumu ya maandalio – sharika nyingi ziliitumia Alhamisi kwa shughuli hii.

## 2. Elimu ya Kikristo ni Taaluma

Mafundisho ya kikristo kama wajibu wa wachungaji ni hatua moja, lakini mafunsdisho sahihi, yanayofundishwa kwa utaratibu na weledi ni jambo la pili. Hii ni kusema, Elimu ya Kikristo ni taaluma. Kama Mchungaji, haitoshi kutoa majibu rahisi kwa maswali magumu – kama Mwinjilisti wa kujitolea. Mchungaji mmoja mgeni alisema kilichomshangaza sana hapa Tanzania ni majibu rahisi yaliyokuwa yanatolewa na Wachungaji na wahubiri kwa maswali magumu. Watheologia wengi wana majibu karibu kwa kila swali, hata kama ukweli ni kuwa duniani kuna maswali mengi kuliko majibu.

Ni wajibu wa watheologia kuwasaidia washarika kuishi na maswali. Maisha ni pamoja na kuishi na maswali kuliko kuwa na majibu. Mtu akisema anaumwa ebola au kansa na hana hela ya matibabu, basi Mchungaji anaweza kumwambia asihofu, anaita kikundi cha maombi na kukiambia "mfanyieni maombi huyu" – haulizi hata ni hospitali gani imetoa vipimo hivyo, au kansa imefikia hatua gani: unaweza kusikia tu "funga macho tuombe."

- Mfano wa Mchungaji huyu wa zamani (nahisi siyo wa lutherani) aliyekwenda ICU unaonesha utayari wa huduma usiokuwa na weledi. Alikwenda hospitalini kuwaombea wagonjwa, akaingia hadi ICU, ghafla ameshamwekea mmoja mikono tayari, yule mgonjwa ni baba analalamika kwa mikono na miguu maana sauti haitoki, akionyesha kuwa baba Mchungaji amekanya waya wa oksijeni na ni hatari kwake, ah, ye mzee anaendelea kupiga tu, "Baba katika jina la Yesu". Akaandika kikaratasi "umekanyaga waya wa oksijeni, ninakufa" baba Mchunagji sijui alifungua macho kidogo akakiona kile kikaratasi, akakichukua, akakiweka mfukoni bila hata kukisoma, akaendelea kupiga sala, mpaka anamaliza, na mzee alishafika Yerusalem siku nyingi.

Sasa alimfunga macho vizuri na mdomo lakini nahisi juhudi yake na moto wa maombi vilimuwahisha mzee wetu Yerusalemu mpya. Juhudi kubwa bila maarifa ni sawa na kupoteza muda. Haitoshi kuwatisha wakristo kwa mambo magumu kuwapa vitisho “hiyo ni dhambi” au “Biblia imekataza” bila kufafanua na kufikiri umemaliza. Huwezi kuulizwa kwanini tunabatiza ujibu kwa kusema “usipobatizwa ni dhambi”. Kujibu hivyo kungekuwa uvivu wa Mchungaji. Ni lazima ueleze na kufafanua.

- Mimi mwenyewe natokea kwenye vikundi hivi vya uamsho – nilikuwa wale “ndugu wa mzigo” – wanamaombi. Siku moja mmisionari mmoja alituhurumia tukiomba akatufuata Chapel akasema “inatosha sasa, amesikia.”

Chagamoto za kimazingira na utandawazi zinafanya kazi ya Elimu ya Kikristo isimamiwe zaidi na wachungaji, tena wafanyao kazi kwa weledi na sio kuwaachia walei, wainjilisti na watu wa kujitolea usharikani.

Ni wazi kuwa, Mchungaji kama mtheologia na mwalimu wa Elimu ya Kikristo lazima awe mtu anayejifunza na kujinoa kila siku. Zipo changamoto zinazoonyesha umuhimu wa Mchungaji kuendelea kujifunza, kujinoa kimafundisho, sio lazima kusoma theologia zaidi, lakini kijinoa kwa elimu ya kawaida. Kwa maneno mengine, kubarikiwa kuwa Mchungaji siyo mwisho wa kujifunza, kama changamoto zifuatazo zinavyoonesha:

- Kwenye mkutano wa kiroho nilipokuwa mwanafunzi wa theologia mwaka wa kwanza, Wachungaji wote tulikaa mbele kama kawaida. Mhubiri akauliza katikati ya mahubiri kwa nini ndoa ifungiwe kanisani - kibiblia au kitheologia? Mimi sikuweza kujibu na wala wale wachungaji wazee hawakuweza. Tuliaibika pale.
- Kufundisha kipaimara kwa kutumia fimbo hakujapitwa na wakati kweli? Inatosha kweli kusema „Usimnyime mtoto wako mapigo, maana ukimpiga kwa fingo hatakufa,“ (Mithali 23:13)
    - Mwanafunzi mmoja wa kipaimara wakati fulani aliuliza: “Baba mchungaji kwa nini Mwinjilisti wetu wakati wa somo la kipaimara anakuja na fimbo darasani, anaamini lazima tutakosea, si aitafute fimbo tukikosea?”
    - Hii labda itakumbusha hadithi ya zamani kwenye gazeti juu ya mzazi aliyemchapa mtoto wake kila mwisho wa mhula maana siku hiyo matokeo yalikuwa yanatolewa na alikuwa anakuwa wa mwisho. Alimchapa mihula kadhaa, siku moja alipaswa kusafiri kabla ya siku ya kufunga shule. Ilibidi amwite, akamtandika, akamwambia kesho matokeo yakitoka nitakuwa sipo, ndio maana nimemaliza kazi yangu ya kesho leo leo. Alimtandika akiamini kesho yake matokeo yatakuwa mabaya na watakuwa wamemalizana mpaka mhula mwingine. Fikiria matokeo yalipotoka, mtoto alikuwa katika nafasi nzuri na walimu waliandika barua kwa mzazi kumpongeza mtoto wake ameanza kujifunza.
- Njia/ mbinu za ufundishaji (methodology) ni changamoto kubwa! Ni njia tunazopaswa kujifunza, hazishuki kutoka mbinguni. Kufundisha kunahitaji taaluma – ni zaidi ya kusema roho anafanya kazi ndani yangu.
- Labda changamoto nyingine za kufundisha ni kubwa zaidi, zinazolingana na mazingira na matukio. Juzi Mchungaji mwenzetu (yupo hapa leo nimemwona) alishangaa anaandikisha mtoto wa kipaimara - mjamzito. Alijiuliza, nitamchanganya na watoto wengine? Nitamfundisha tofauti na wenzake? Nitamfundishaje? Kwa wachungaji wengine hapa labda hili siyo jambo geni sana. Mchungaji wa kawaida angeanza

kumfundisha kwa kumweleza jinsi alivyovunja amri ya sita – usizini. Na anapaswa kujutia ujauzito/ dhambi hiyo.

Yule binti alivyomsikia baba Mchungaji anazungumzia mambo ya kujutia ujauzito alishtuka sana na kujibu: "Baba Mchungaji nilifikiri unamshukuru Mungu pamoja nami kuwa kuna kiumbe cha Mungu ndani yangu kinachokua… Mimi sijutii kuwa mjamzito, namshukuru Mungu kuwa siyo tasa na sasa Mungu amenipa karama ya uwakili wa kutunza kiumbe chake. Nimekuja kipaimara kutafuta baraka katika hali niliyonayo! Siyo kujutia." Hii imetokea usharikani hapa hapa KKKT kwetu – Mashariki na Pwani.

Hapo sasa baba Mchungaji alifahamu kumekucha, alifahamu pia kuwa zana na silaha za zamani zinafikia mwisho. Tunahitaji zana mpya! Swali ni: Tunahitaji Elimu mpya ya Kikristo? Biblia siyo ile ile? Luther alisema: "Die Bibel ist nicht antik, sie ist auch nicht modern, sie ist ewig" - **Biblia siyo ya zamani, siyo ya kisasa, ni ya milele."**

Sasa kuna mafundisho mengi na mapya kila mahali. Mahubiri na mafundisho (Elimu ya Kikristo) ni soko huria. Ni Mchungaji anayejiongeza kitaaluma tu anaweza kukabiliana na changamoto mpya za mafundisho kama haya.

Huko nje utafundishwa:

- Ujasiriamali kwa kuwekewa mikono na kuambiwa "pokea" – "pokea ujasiriamali kwa jina la Yesu". Nilipouliza watheologia kadhaa juu ya hali hii wengine wakasema ni sawa, maana ujasiriamali maana yake ni ujasiri juu ya mali. Ujasiri mtu huombewa. Nikakumbuka, huko chuoni kwetu somo la "Ujasiriamali (interprenuarship) ni somo la mihula (semester) kadhaa. Lakini hawa wanapata kwa mara moja tu.
- Nguzo za ukristo ni pamoja na kwenda hija - Yerusalemu, tumekuwa kama wanasiasa – "ukitumbuliwa" unaenda hija – 'break' ni Yerusalem.
- Kuwa kama unabatiza watoto wawili wa familia moja ni lazima uulize katika hao kama mmoja ni mzaliwa wa kwanza –"lango" - maana huyo atastahili kukombolewa na utatumia liturgia tofauti.
- Elimu ya Kikristo ni juu ya Shetani? Huwa ninauliza watu, baba Askofu wako anatamka shetani mara ngapi kwenye mahubiri? Kuna makanisa ambayo shetani, nguvu za giza na mapepo ndio mradi – 'project' yao. Siku vikiisha, watarudi Lutheran na RC, maana walitoka huko.

- Watu wanafundisha elimu ya shetani. Akili za waumini wengi zimetekwa sasa na nguvu hizi. Ukiona watu wamesinzia kanisani huwezi kuwaamsha kwa kusema hata kama ni kwa sauti kubwa kwa kusema: "Mungu Baba, Mwana na Roho Mtakatifu".

  Wanaweza kuendelea kusinzia. Ukitaka waamke sema hata kwa upole kabisa: "Na hizi nguvu za giza ee Bwana, tunazifunga vitita vitita, na kuzitosa kwenye vilindi vya bahari… na pepo la ajali tunalikemea." Hapo hata watoto wataamka wakisema "kwa jina la Yesu!"

  Maeneo mengine duniani hayana shetani mkubwa hivi. Au shetani anapenda rangi nyeusi zaidi? Kuna uhusiano wa mapepo na Waafrika? Kuna utafiti unaendelea, mbona kwenye

mikitano ya kiroho mapepo yanaangusha wamama tu zaidi? Kule Dar es Salaam hayaangushi wamama wengi wasomi na wenye heshima…? Yanashughulikia kada fulani.

Nimeishi miaka 7 na nusu nje ya nchi bila kusikia neno shetani – karibu “ningelimisi” - najiuliza nimekosa nini mpaka hapo? Nilipowashuhudia wenzangu jambo hili waliniambia shetani huko ulaya anatumia mbinu ya kuwa hayupo, anajifanya amelala. Mwenzake aliyekuwa pembeni akajibu: „Sasa wamwamshie nini? ... Ukimwamsha aliyelala utalala wewe? Chuoni tulitaniana kuwa shetani anamzuia mtu kuokoka kwa kujifanya hayupo, akiona anamshindwa anamsukumia kwenye wokovu – mpaka mtu anakwama kwenye matope ya “kuokoka”.

Ni rahisi kuona waimbaji wanatunga nyimbo kuhusu shetani wakiamini ni nyimbo za Injili – “shetani nipite,” nk.

- Kuwa hakuna tofauti ya mafundisho ya kiyahudi na ya kikristo. Watu wote lazima watoe zaka. Ni sharti. Na ukitaka kukorofishana na Wachungaji ufundishe tofauti. Mchungaji mwenzangu aliyefundisha kuwa zaka ni mafundisho ya Kiyahudi – japo hayo ndiyo mafundisho ya kweli, karibu angeambulia kichapo kutoka wa watumishi wenzake.

Sababu zinajulikana, kwa nini ukweli huu haupokelewi - Gari analoendesha mchungaji lilinunuliwa kwa zaka, hata kama sio mafundisho sahihi – lakini zaka inalipa. “Yesu hakumwambia yule tajiri akauze vyote alivyokuwa navyo na kisha atoe zaka…” Mafundisho sahihi ya kikristo ni kutoa vyote kama Bwana wetu – hili ni somo jipya linalohitaji muda.

- Kuwa Biblia, Mungu, Kanisa na Injili ni kitu kimoja (you can use all these nouns interchengiably).
    - Kukaza kidogo hilo: Professor Alfred Loisy wa Ufaranra anakumbukwa kwa sentensi yake muhimu: “Yesu alifundisha kuhusu Ufalme wa Mungu, kilichotokea ni kanisa.”
    - Kwa ulaya sensteni hii ni mashuhuri sana na wao kwa itikio wanasema: “Yesu ndiyo, lakini kanisa hapana!” Wao hawajali maana wanaona mtikisiko mkubwa wa kiimani unaoendelea sasa Ulaya utaliletea kanisa hasara kubwa, lakini sio Mungu. Ni kusema, kuna wakati kanisa linapata hasara, na sio Mungu.

    Ni kutaka kuuliza: Yesu akija sasa hivi na akatakiwa kujiunga na kanisa moja tu, angelienda lipi? Naamini Lutheran! Mwalimu wetu alituambia Yesu hana vigezo vya kuwa mchungaji wa lutherani, angalau kwa dayosisi kadhaa isingewezekana, maana hajapita kwenye chuo kinachotambuliwa cha theologia. Nchi nyingi zina mitihani ya kitaifa ya theologia.

    Mwanafunzi mmoja alisema kwa nchi yao hata Bwana Yesu mtihani wa Theogia kwa mara ya kwanza asingefaulu maana wanafunzi wote kwa mara ya kwanza hufeli. Maprofesa “wangemsapisha” Bwana wetu kwanza, na akifanya mara ya pili angefaulu.

    - Labda kanisa na Mungu vinakuwa wazi kwa mfano huu: Mtu mweusi alikwenda kwa Mchungaji zamani kule New York akimwomba kama angeliweza kujiunga na kanisa lake lililokuwa na watu weupe zaidi, baba Mchungaji alimjibu: “oh nimepokea ombi

> lako, nitakwenda kuomba kwa Mungu kama utaweza kujiunga na usharika huu". Yule Mwafrika naye kule nyumbani kabla ya jibu la Mchungaji aliendelea kuliweka jambo hilo mikononi mwa Mungu. Usiku Mungu alimjibu yule Mwaafrika akisema: "Usihaingaike na hilo kanisa, mimi mwenyewe nahangaika kuingia hilo kanisa kwa miaka kadhaa mpaka sasa bila mafanikio. Kama mimi sijafanikiwa, sembuse wewe?"

Huko hata maana ya miujiza imepotoshwa, watu huandaliwa kusema wameponywa, wamefufuka n,k. Wanaotembea wanapewa muujiza wa kutembea.

Nasisitiza bado, Mchungaji kuwa na wito, nia njema, juhudi na moto wa injili haimaniishi ni Mchungaji mwenye mafanikio – anahitaji maarifa na weledi – nia njema haimanishi kazi nzuri. Katika kitabu cha Matendo ya Mitume tunasoma habari ya Apollo, mtu mwenye wito, nia njema na juhudi kubwa ya kufundisha - alikuwa na maarifa na akayafundisha, yalikuwa lakini maarifa ya zamani ya ubatizo wa Yohana, kumbe wenzake muda mrefu tu wanabatiza kwa Roho Mtakatifu.

Mpaka alipokutana na akina Pricilla na Akila ndipo alipogundua anapaswa kujinoa kwa upya juu habari ya ubatizo wa Roho Mtakatifu (Matendo ya Mitume 18: 24-26). Hivyo wito na moto wa kazi ya injili ni jambo moja, ni kama Apollo, lakini maarifa na weledi ni jambo la pili na la muhimu ili kuleta matokeo chanya. Ni katika mazingira haya sentensi hii ina maana: "Mimi ni Mchungaji wa mshahara ninayewazidi hawa wa wito kiutendaji." Na ndio maana hata kama una wito mkali kiasi gani, unapelekwa chuoni kwanza - uelimishwe.

Nilimtishia mtunza hazina katika usharika wa usharika wangu niliokuwa nafanya kazi kuwa mimi ni hawa wa mshahara - ukiniwekea mshahara tarehe 30 sikilizia uinjilisti wa nyumba kwa nyumba tarehe moja na kuendelea - akanipa mshahara. Sasa msiulize ni usharika gani, kuna sharika mtunza hazina ana nguvu kuliko Mchungaji – hapa mimi nilikuwa Mchungaji mwenza wa Mchungaji mwenza. Ni mimi peke yangu sijaacha mshahara kwenye huo usharika.

Elimu ya Kikristo ni muhimu kwa ufahamu wetu binafsi na kwa lengo la kusaidia wengine – kufundisha. Huwezi kwenda kufundisha kitu ambacho wewe mwenyewe unatakiwa ufundishwe. Shuleni mwalimu anaweza kufundisha somo jipya ambalo hakuwahi kulisikia, akaangalia mtaala (syllubus) na kujisomea akafundisha.

Lakini, je? Mtu asiyekuwa mkristo anaweza kufundisha Elimu ya Kikristo? Yeye ni Mbudhisti au Shekhe, akasoma "syllubus" yetu ya Elimu ya Kikristo na kuanza kufundisha? Mheshiwa rais kama anatakiwa kutoa hotuba mahali na ghafla akashindwa kutuma mtu kutoka serikalini au wizarani kusoma hotuba ile. Elimu ya kikristo ingemhitaji mchungaji kutuma mchungaji mwezake – siyo ilimradi mtu ni mtu.

Swali kubwa na muhimu la kitheologia na kwenye elimu ya dini ni kuuliza tofauti iliyopo kati ya: mtu anapochunguza dini yake na anapochunguza dini nyingine - kuangalia dini nyingine ukiwa mkristo au ukiwa huna imani katika dini yeyote – 'neutral'. Elimu ya Kikrsito inafundishwa na wakristo – tena walioiva kwenye ukristo. Wachina wana methali isemayo: "Picha moja nzuri ni bora kuliko maneno elfu moja."

Mpaka hapa nilitaka kusema mambo mawili tu muhimu:

i. Kufundisha Elimu ya Kikristo ni wajibu mkuu wa Mtheologia/ Mchungaji maana yeye ni wakili wa mafundisho sahihi ya Neno la Mungu.
ii. Pia ni wajibu wa Wachungaji kujinoa kila wakati - maana Mchungaji ndiye "rejea" (reference) ya kitheologia kwenye usharika.
    - Wito: Makumira iandae utaratibu wa kuendelea kunoa Wachungaji – angalau muhula mmoja baada ya muda fulani – mfano baada ya miaka saba – tupate pia "sabathical leave" ya Wachungaji.
    - Makanisa mengine wachungaji wana nafasi kila mwaka kujiendeleza kwa kufanya kozi fulani fulani fupi kwa njia ya mbalimbali – "online courses" ambayo wahadhiri wa vyuo vyetu wangaweza kuzisimamia.

Dayosisi za Kaskazini Kati, Iringa, na Kusini zina kitu kinaitwa ETE – Elimu ya Theologia kwa Enezi - kule Arusha wanaita TEE – "Theological Education by Extension" mahali ambapo tunaweza kujifunza. Hapa Wainjilisti wanajinoa na sisi Wachungaji tunawafundisha - tunawanoa.

Mwika Bible College walikuwa na juma la kusifu na kuomba ambapo wanafunzi wa zamani walikutana na kuendelea kunolewa.

**3. Umuhimu wa Elimu ya Kikristo**

Katika ufundishwaji wa Elimu ya Kikristo utagundua wafundishaji wana malengo kadhaa tofauti.

i. **Wapo wanaotaka Ukristo usife.**

Tulipokuwa darasa la theologia, mmoja wetu alisema "ukristo hauwezi kufa maana ni kazi ya Mungu." Wote hata mwalimu tulikubali, maana nani anaweza kuangusha kazi ya Mungu. Ghafla, mwanafunzi mwenzetu aliuliza: "Mbona ukristo nchini Misri ulikufa?" Hakukuwa na jibu kwa muda maana kila mtu alijua Misri sasa ni nchi ya kiislamu, kikanisa kidogo cha kikopti kilichopo hakina nguvu pamoja na ukweli kuwa Injili kwa Afrika ilifika kwanza Misri.

- Kumbuka pia kuwa mtoto Yesu alifanya safari ya kwanza ya nchi za nje nchini Misri.
- Tunasoma Mtakatifu Marko alifanya umisionari huko Misri mara tu baada ya Yesu kupaa.
- Mababa wakuu wa kanisa wanatoka Misri na hata majadilaino makubwa ya kitheologia yalifanyikia Misri.

"Ilikuwaje kanisa hili likafa?" Wengi huuliza hivyo. Watheologia wengi wanalaumu kanisa la Misri kwa kutoweka mipango mizuri ya Elimu ya Kikristo ndiyo maana ukristo ukaanguka. Juzi nimekutana na sababu nyingine, kubwa iliyoliua kanisa la Misri. Wale wa historia ya kanisa wanaweza kusema zaidi. Mwandishi mmoja, Gehard Gasper, mmisionari kutoka Ujerumani aliyefanya kazi kule Bukoba miaka ya sitini anaandika katika kitabu chake kuwa mchanganyiko wa siasa kanisani vililiangusha kanisa la Misri.

Baada ya Kanisa kushika pia dola kwenye historia – askofu akawa pia Kaisari na baada ya kugawanyika utawala huu - kule Rumi na Konstantinopole (Istanbul kwa sasa), kule Uturuki ya

sasa, Misri kisiasa na kidini ilibaki kuwa koloni la kisiasa na kidini la Konstantinopole. Kodi na mambo ya utawala yaliwalemea.

Uislam ulipokuja nao kwa mfumo huo huo wa dini na utawala katika kofia moja, wamisri waliona ni bora kujiunga na utawala wenye nafuu … hata kama ni uislam! Wakristo wenzao wa Konstantinopole iliwatoza zaidi – wakasema heri uislamu wenye kodi na masharti machache. Siasa na dini! Hii labda inatufanya tuwaze vizuri.

Lakini siyo Misri tu ambako ukristo ulikufa. Hata kule Uturuki hakuna ukristo tena. Huko ndiko maaskofu na viongozi mbalimbali walikaa na kujadili mambo ya kiimani na kutokeza Imani ya Nikea. Si kitu cha kuaminika kuwa Waraka wa Mtume Paulo kwa Waefeso ungeweza kuandikwa waraka wa Mtume Paulo kwa Waturuki. Waefeso wa wakati huo ni miongoni mwa Waturuki wa sasa. Kwa sababu ya siasa Efeso na miji yote iliyokuwa ya Kikristo kwa wakati ule, sasa ni nchi ya Kiislamu. Uturuki yote ni nchi ya Kiislam. Makanisa yetu yamebakia kuwa magofu na mengine yamefanywa kuwa misikiti.

Waefeso, watu wale Mtume Paulo aliowaambia: "Tunaokolewa kwa neema kwa njia ya imani" leo hawaruhusu kujenga kanisa la Yesu Kristo nchini kwao. Hata kama kuna wamissionari, wakikutwa wapo hatarini kuuwawa. Wamisionari huko wanatakiwa kuishi kama watalii, yaani katika paspoti zao hawaruhusiwi kusema wanahubiri Injili. Siasa na dini, siasa na injili. Wengi wanapambana kufundisha juu ya Ukristo ili usife kama ilivyokuwa Misri na Efesso.

ii. Tafiti nyingine zinaonyesha kuwa kuna wazazi wanapeleka watoto wao kwenye shule zenye mchepuo wa kufundisha elimu ya dini ili watoto waongezee pia elimu hii ya dini – ukristo. Mkazo hapa ni kuwa huwezi kuielewa dunia kama huelewi dini – hasa ukristo na uislamu na maendeleo yake mpaka sasa. Hivyo, kuna wanaofundisha Elimu ya Kikristo wakiwa na mkazo wa kuongeza elimu juu mambo yaliyopo duniani.

iii. Zipo jamii zimeishi na ukristo kwa muda mrefu, na Ukristo ukawa sehemu ya utamduni wao. Wao wanatamani usife hata kama hawana sehemu kubwa tena kanisani. Ni katika kanisa hilo babu na bibi wamezikwa, baba na mama yao wameona hapo, wao wakabatizwa hapo, wakaenda kipaimara hapo, wameolea pia hapo, hili kanisa ni sehemu ya historia yao. Hivyo wangetoa fedha na sadaka ili historia yao iwepo.

Miji mingi duniani hasa Ulaya makanisa ni sehemu ya historia ya miji na ndio maana hata gharama za utunzaji wa makanisa haya zinabebwa na kodi za wananchi. Idara ya utamaduni inatunza majengo ya zamani pamoja na makanisa. Au hata kwetu ni hivyo; kwamba mtoto anabarikiwa kama sehemu ya utamaduni wa mahali, utakuwaje hujabarikiwa wakati watu wote wamebarikiwa? Mchungaji mmoja amefananisha "kipaimara na jando" katika andiko lake.

iv. Jamii nyingine zinahisi watu wasipofundishwa ukristo au elimu ya dini jamii hiyo itaishia kuwa jamii isiyokuwa na maadili. Ili kupata jamii yenye uadilifu na inayojadili ustawi ni lazima ifundishwe elimu ya dini – Elimu ya Kikristo. Hata wakoloni waliwasaidia wamisionari kueneza Injili ili Injili ilainishe watu mioyo wasipinge ukoloni. Kwa sehemu nyingine ilikuwa ni lazima wamisionari watangulie kwanza. Ndio maana ya sentensi hii: "Flag followed the Bible" – "Bendera ilifuata Biblia". Sentensi ya Jomo Kenyatta inaweka wazi hali hii wakati wa kupigania

uhuru aliposema: “Wazungu walipokuja walitufundisha kuomba kwa kufunga macho, tulipofungua tulijikuta tumeshika Biblia na wao wameshika ardhi.” Hata hivyo mwandishi mmoja wa Kiafrika amemjibu Jomo Kenyatta kwa kusema: “but we have the better part” – “lakini sisi tumeshika sehemu iliyo bora zaidi”. Tumebaki na sehemu nzuri wakati ardhi imeondoka? Ndiyo, Injili inaweza kurudisha ardhi.

Kwa kujali mchango wa Elimu ya dini katika kujenga jamii imara kimaadili baadhi ya nchi huajiri au hulipa walimu na Wachungaji wa Elimu ya Dini ili wafundishe. Mfano kwa nchi ya Ujerumani, Wachungaji wanaofundisha Elimu ya Kikristo shuleni wanalipwa na serikali. Serikali isingekuwa inasaidia hivi, ukristo ungekuwa umeshafutika Ujerumani.

Habari za Yesu watu huzisikia kwa mara ya kwanza katika shule za awali (kindergarten), shule za msingi na sekondari. Kanisani wengine huhudhuria krismasi na pasaka tu. Wanafunzi wa kipa imara hulazimishwa kuhudhuria angalau mara kumi ili waweze kubarikiwa. Na wakisha barikiwa wengi hawaonekani tena.

Usharika niliofanya kazi wenye washarika 8,400, haukuwa na Shule ya Jumapili yenye watoto zaidi ya 10. Mara kadha walimu wa Shule ya Jumapili walikuwa wengi kuliko wanafunzi. Mara nyingine ni watoto wetu tu walihudhuria Shule ya Jumapili, na tulipoondoka, walibadilisha utaratibu, “Sunday School” ni mara moja kwa mwezi. Katika mazingira kama haya, ukristo utabaki tu kama watafundisha shuleni. Hilo wanalifanya kwa nguvu na kwa msaada wa serikali. Hapa kuna jambo la kujifunza: kutumia kila nafasi - “chance” - na upenyo vizuri kupeleka ujume wa Injili. Dini shuleni ni nafasi ya pekee – tuitumie vizuri.

Serikali ya Tanzania hailipi waalimu wa dini mishahara. Lakini kuna taarifa kutoka serikalini - “secular” - kuwa somo la dini lifundishwe na taarifa itolewe kwa vipindi visivyofundishwa. Kwa kuwa mchungaji mara nyingi hafiki kufundisha dini shuleni, kipindi chake wanafunzi wanakipenda maana wanacheza nje au kuomba ruhusa kwenda kufanya wanachotaka.

Wakati wachungaji wakitupiana mpira na kuulizana mwaka mzima shule fulani inatunzwa na usharika gani, au na Mchungaji gani, watoto wanaendelea kukosa elimu hii muhimu. Wapo pia watoto wanaopenda kipindi cha dini na hupunjika sana Mchungaji asipofika. Kuna Wachungaji pia wanaotenga siku maalumu hata kwa ajili ya shule ya chekechea pale usharikani. Hawa wanajua usharika huanza na watoto.

- Kuna wanaofundisha Elimu ya Kikristo kwa kuwa ni “utume mkuu” kwetu. Wanafundisha kama hatua ya kuujenga Ufamle wa Mungu duniani. Wanaamini ufalme huu ulishakuja, upo na unahitaji kukamilishwa – nasi tumealikwa kushiriki kazi ya kuukamilisha.
    a) Hawa wanaamini Elimu ya Kikristo ni elimu inayomweka mtu huru – “Mwana akiwaweka huru mnakuwa huru kweli kweli.” Wanataka habari hii njema ya uhuru na neema iwafikie wote.
    b) Ni kundi hili pia linaloamini kuwa linapaswa kusaidia watu kuishi na maswali waliyo nayo na siyo kuwapa watu majibu – wasiyokuwa nayo.
    c) Ni kundi hili linalotoa elimu kuwa “furaha” sio “matokeo” – ni “uchaguzi.” Furaha ingekuwa matokea ya utajiri au vipawa basi furaha ingekuwa jambo la

watu wachache. Furaha ni uchaguzi – kila mtu akitaka kuwa na furaha anaweza. Mfano, mtu mmoja ambaye hakula siku saba mfululizo kwa sababu ya kukosa chakula alichagua kuwa na huzuni. Mwenzeke alichagua furaha maana alikuwa hajala siku saba kwa sababu ya mfungo.

**4. Chimbuko la Elimu ya Kikristo**

**a. Elimu kwa ujumla**

Kabla ya kuuliza elimu ya kikristo ni nini mtu angeuliza elimu ni nini? Mtheologia mkongwe wa kanisa letu, Prof. Festos Bahendwa, anafundisha katika kitabu chake "Elimu ya Kikristo" kuwa: "Elimu ni mabadiliko ya mtu. Elimu ni mabadiliko yanayoanza mtoto azaliwapo na kuendelea mpaka kufa kwake."

Akifafanua zaidi anakaza kuwa Elimu inajumuisha mambo yote (yaliyopangwa kufundishwa na yasiyopangwa) ambayo mtu hukutana nayo na kumbadilisha. Yale mtu akutanayo nayo, iwe shuleni au kwenye maisha, na hayakumbadilisha, hayo sio elimu kwake. Ndio maana kuna tofauti ya kusoma na kuelimika, kuna wasomi wengi lakini walioelimika ni wachache.

Hivyo elimu ni mkusanyiko wa yale yote ambayo mtu amejifunza kwa njia mbalimbali na yakamletea mabadiliko yeye binafsi. Kuelimika ni kubadilika kwa kupata tabia mpya. Mabadiliko ni tabia ya binadamu. Mwandishi wa Kifaransa, Francis Picabia, anaandika, "Kichwa ni cha mviringo, ili kuwaza kuweze kujibadilisha kila upande". Elimu ni mabadiliko ya fikra, utu na tabia. Ndio maana kipimo cha elimu ni mabadiliko, siyo maneno mengi au vitabu.

Wale ambao ni waalimu hapa watakubaliana na mimi kuwa huko kwenye fani ya ualimu kuna nadharia chungu nzima juu ya elimu na jinsi maarifa yanavyoweza kurithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine. Sithubutu kuzigusa nadharia hizo maana huo siyo uwanja wangu, maana hata elimu ya kikristo tu siyo uwanja wangu. Ndio maana nazungumza kwa woga nikijua wazee wa "practical theology" wapo hapa. Lakini, ili tusitoke kabisa bila nadharia nataja sentensi kadhaa zinazoendana na nadharia hizi:

**i. Uhusiano wa Somo na Jaribio (Lesson and Test/ Exams)**

Maneno ya mwandishi wa Kimarekani, Tom Bodett, kuhusu tofauti kati ya maisha na shule yanafahamika vizuri na wengi wetu. Bodett anauliza: "The diference between school and life? In school you are taught a lesson and then given a test. In life you are given a test that teaches you a lesson" – "Tofauti kati ya shule na maisha? Shuleni unafundishwa somo na baadaye unapewa jaribio (test). Kwenye maisha unapewa jaribio litakalokufundisha somo."

Nadharia na vitendo – huduma ya Neno na huduma ya matendo. Kwa lugha yetu leo ya "Elimu ya Kikristo ungesema elimu yoyote lazima iguse maisha ya mtu ya kila siku. Makanisa yanachofundisha na washarika wake wanachofanya ni vitu viwili tofauti maana "dogma" zao zilitungwa miaka mingi na hazifanani na hali halisi ya sasa. Watu hawasubiri kufundishwa na Mchungaji kitu cha kufanya, maana maisha yanawafundisha zaidi.

Ndio maana kwenye mahubiri utagundua wengine wanaanza na mfano wa maisha halisi (wana anza na jaribio - testi) na wanarudi kwenye somo. Wengine hubaki kwenye Neno tu "solar scriptura" na washarika wao hawajifunzi chochote – hawabadiliki.

**ii. Kufanya kwa "usahihi" au kufanya "jambo sahihi"**
Tunafundisha watu kufanya mambo sahihi au kufanya mambo kwa usahihi?

- Watawala - "Managers" wanafanya mambo kwa usahihi, jinsi sheria inavyosema, jinsi utaratibu unavyosema – hata kama sio jambo sahihi.
- Viongozi - "Leaders" wao hufanya jambo sahihi – hata kama itabidi kutolifanya kwa usahihi – "the end justifies the means"!
- Katika Elimu ya Kikristo watu wengi wanafundisha "Biblia na uyahudi" kwa usahihi mkubwa – unaweza kuwaita "Bible managers." Jambo sahihi lisingekuwa kumhubiri Kristo? Kuna tofauti kidogo, ukibaki kuihubiria mifupa kama Nabii Ezekiel anavyosema inakuwa ngumu kupata kitu, wasikilizaji wako wanaweza kushindwa kufaulu majaribio na mitihani ya maisha ilizopo mbele yao.

**iii. Ukweli na mabadiliko**
Ukweli ni nini? Yesu anasema "Mimi ndiye njia, kweli na uzima" (Yohana 14:6).

- Tena tunafahamu juu ya "Hakuna jina jingine chini ya mbingu tulilopewa wanadamu litupasalo kuokolewa kwalo" (Matendo 4, 12).
- Yesu alisema "Sikuja kuitangua torati bali kuikamilisha" (Mathayo 5:17)

**a. Ukweli haubadiliki**
Wapo wanaoamini kuwa ukweli haubadiliki. Ndio manna kazi ya mwalimu ni kuuchukua ukweli huo wa milele na kuubandika kwa mwanafunzi – inaitwa "banking" au "copy and paste!" Hii labda ina ukweli fulani kwa masomo ya sayansi na mahesabu. Kwa masomo ya kijamii na kiroho ni kama kusema Biblia ndiyo ukweli, hivyo unaisoma tu ilivyo mfano: "kanisa la zamani liliuza viwanja, nasi tuuze hata kama ni kule Masaki; Mtume Paulo hakuoa, nasi tusioe au tukafukuze tulioa, mitume walikaa Yerusalem wakasubiri "percent", na sisi tusibiri "percent" sharikani au ofisi kuu, nk.

Hata hivyo hakuna hasara kufundisha baadhi ya mambo kwa mtazamo huu kama "Sala ya Bwana", Imani ya mitume, ahadi ya ubatizo, Zaburi 23 nk. Sala ya jioni, ya asubuhi na ya chakula.

Wale walioweza kushika kwa kichwa sala na mistari kadhaa ya Biblia imekuwa akiba yao ya baadaye wakiwa wenyewe njiani, hospitalini, wakati wa hatari, nk. Mambo uliyoyafanya ukiwa mtoto utayafanya tena ukiwa mtu mzima. Ukifikia miaka ya uzeeni mambo uliyojifunza kwa kichwa yanakusaidia maana unaweza kuyakumbuka zaidi: Sala ya Bwana, Neema, Ukiri wa Imani, nk.

**b. Ukweli hubadilika badilika.**

- Kwamba ukweli hubadiliki badilika ilimchanganya Luther kidogo na hoja yake ya "Neno tu" alipoambiwa ni dunia ndiyo inazunguka na sio jua kama tusomavyo kwenye maandiko kuwa Joshua alisimamisha jua (Yoshua 10:12). Luther aliondoka bila kumalizana na jambo hili yeye mwenyewe lakini alikubali kuwa biblia siyo ya kisasa, japo ni ya milele.
- Hapa mkazo ni kuwa elimu ni maisha yenyewe na siyo somo na maandalizi ya namna ya kuishi. Hapa kufundisha kunapaswa kuwe kwa namna ya kutatua tatizo liliopo kuliko

kuandaa kufundisha somo lisilokuwepo. Labda maadili (what is wrong and what is right) yapo kwenye ukweli unaobadilika.

- Maadili ni jambo la jamii fulani tu. Jambo lolote la kimaadili limapimwa na jamii husika na haliwezi kufanywa ni jambo la kufanana kwa jamii zote.
    - Mfano wa wanaume kuvaa hereni masikioni. Hata mimi ni jambo linanikera. Nilipoona Mchungaji wa kizungu amevaa nilihisi ni 'freemason', lakini pembeni yake kulikuwa na Mchungaji wa Kimasai akiwa amevaa hereni kubwa zaidi masikioni, sikuona ni 'freemason'.

      Nilijiuliza: Je, siyo kwamba hatuoni kweli kila wakati kwa sababu tunaona tu kile tunachotaka kukiona? Hatuoni vitu halisi, utamadani wetu umetufanya – umetu-"shape" namna ya kuona. Tunaona tulivyofundishwa kuona.

    - Mfano wa mtoto na mama yake unatufundisha. Anamuuliza kijana wake wa kiume aliyetoka Ufukweni: "Halo John, huko ufukweni, kulikuwa na wasichana pia?" "Sijui", alijibu. Alipoulizwa kwa nini hajui, alijibu: "Ningefahamu je? Hakukuwa na mtu amevaa nguo." Hii ni kusema, mambo mengi ya kimaadili hayana uhusioano na ukristo, yana uhusianao na tamaduni zetu.

      Wengi wetu hapa huhubiri Unyakyusa, Uchaga na Umasai tukiamini tunahubiri Injili. Wengi kwa kutojua hujikuta wamefanya utamaduni wao ni sehemu ya ukristo.

    - Hata hivyo Injili imepitia tamaduni mbalimbali mpaka inatufikia, Uyahudi, Uyunani, Urumi, ulaya, Uchaga nk mpaka ifike Sonjo. Mfano kwenye harusi tunafundisha Uyunani tunapomwambia bwana na bibi harusi: "Baba atakuwa kichwa na mama mkia?"

- Harusi siyo lazima kuvaa nguo nyeupe, huo sio uzungu kweli? Wachungaji wa zamani walivaa hata vazi jeusi kama walifunga ndoa ya mwanamke aliyekuwa mjamzito, au mama alinyimwa kuvaa shela kama adhabu. Ulikuwa uonevu mkubwa tu kwa wamama maana mzee yeye suti yake, awe amempa mama ujauzito au la, baba awe naye mja mzito au la, suti yake haikuguswa. Labda ni wakati sasa wale wa utamaduni wabuni vazi la harusi la kitanzania - tuachane na haya ya kizungu. Lakini watu watakubali?

**c. Ukweli upo ndani ya Mwanafunzi au ya Mwalimu?**

- Kwa Plato mwanafunzi ana ukweli wote na kazi ya mwalimu ni kuuamsha usingizini tu. Labda anafanana na nabii Yeremia anaposema wakati utafika watu hawatahitaji kufundishwa tena maana ukweli watakuwa nao umeandikwa mioyoni mwao. Ubaya na wema ni kama umeandikwa tayari ndani yetu, kwenye dhamiri upo tunausikia. Kuua au kuiba ni wazi kuwa ni vitendo visivyohitaji kufundishwa – ni kuamshwa tu usingizini.
- Kwa Aristotles hakuna kitu kipo kwenye akili isipokuwa kimeingia – kimeingizwa na ndiyo maana ni wajibu wa mwalimu kuingiza ukweli huu. Hakuna mtoto anazaliwa akisema Sala ya Bwana, au akizijua amri, lazima afundishwe.

Mawazo haya yote ni lazima yazingatiwe wakati wa kufundisha na kuhubiri, kila wazo kwa wakati na mahali pake.

Kuna wakati ni mtihani /jaribio linatupata kwanza, halafu somo linafuata, kuna wakati tunatakiwa kufanya jambo sahihi, kuna wakati tunagundua ukweli unabadilika au kukua ndani yetu, kuna wakati mwalimu atawaambia wanafunzi ukweli, kuna wakati mwalimu atajifunza kwao, kuna wakati watajifunza pamoja, maana wote wapo njiani. Mwalimu anapoulizwa njia na wanafunzi na yeye kuonesha kwa kidole, yeye pia huonesha huko anakokwenda. Wote wapo njiani.

**b. Elimu ya Dini ya Kikristo**

Elimu ya Kikristo ni tofauti kidogo na elimu nyingine. Wakati Elimu ya kawaida ni wizara inawatambua waelimishaji, Elimu ya kikristo hutoa walimu wake kwenye kanisa. Wakati kwa jamii ya kawaida siyo kila mtu ni mwalimu, kwa kanisa kila aliyebatizwa amepewa huduma ya kimisionari – "Enendeni ulimwenguni kote…". Hata hivyo, Mtume Paulo anasema wengine wameitwa kuwa walimu – wamepewa kipawa cha zaidi.

Profesa Festo Bahendwa akiandika kuhusu Elimu ya Kikristo anasema: "Elimu ya Kikristo ni jumla ya kazi ya kanisa katika shughuli yake ya kufundisha watu Neno la Mungu na mipango yake ya kuelimisha watoto, vijana na watu wazima katika kuwakuza kikristo."

Elimu ya Kikristo inamaanisha shughuli zote za kanisa za kuhuburi na kufundhisha – sio idara tu, lakini ni pamoja na ofisi ya baba Askofu. Akisema watu wazima inamaanisha pia wazee, maana umri wa kuishi - "life expectance" ya Watanzania sasa inaongezeka kutoka 51 - 65 kwa wanaume na wanawake 54 - 66. Hii bado ipo chini.

Nchi yenye watu wanaoishi muda mrefu kwa takwimu za mwaka 2014 ni Monacco kwa wastani wa miaka 90 na Chad ya chini kabisa 49. Hata hivyo kwa Tanzania wazee wetu wanaishi maisha marefu zaidi kwa sababu ya kuimarika kwa huduma za kijamii hasa huduma za kimatibabu. Hivyo kundi la wazee litaendelea kuwa kundi kubwa zaidi huku tuendako. Jambo hili ni jema lakini ni jambo jipya lenye changamoto zake. Kule Dar es Salaam na Njombe kuna nyumba ya wazee tayari kama ulaya maana mfumo wa familia umeanza kubadilika.

Biblia inatoa picha jinsi Waisraeli na kanisa la mwanzo walivyosimamia Elimu ya Kikristo.

**Agano la Kale**

Katika Agano Kale tunaona jinsi ambavyo mkazo wa mafundisho ulikuwa mkubwa.

- Kwanza Mungu alifundisha mwenyewe: "Zaeni mkaongezeke…, mtailima nchi na kuitunza…"
- Baadaye Biblia inaonyesha kuwa wazazi walibeba jukumu hili la kufundisha.

**Kutoka 12:26-27**

26 Kila wakati watoto wenu watakapowauliza, 'Jambo hili lina maana gani?' 27 Nyinyi mtawajibu,
'Hii ni tambiko ya Pasaka kwa heshima ya Mwenyezi-Mungu, kwa sababu alizipita nyumba za Waisraeli nchini Misri alipowaua Wamisri, lakini sisi hakutuua.'" Waisraeli wakainamisha vichwa na kumwabudu Mwenyezi-Mungu.

**Kumbukumbu: 6: 6-9**
"[6] Wekeni mioyoni mwenu maneno hayo ninayowaamuru leo, [7]na kuwafundisha kwa uangalifu watoto wenu. Mtawasimulia muwapo mnakaa nyumbani au mlipo safarini au mnapolala au mnapoamka. [8]Yafungeni katika mikono yenu na kuyavaa katika vipaji vya nyuso zenu kama ukumbusho. [9]Yaandikeni kwenye miimo ya milango yenu na malango ya miji yenu."

- Wazee na wakuu wa makabila walifundisha juu ya mila na taratibu za kiibada na kijamii kwa taifa lao.
- Baadaye tunaona wafalme kama Daudi na Sulemani na manabii nao walichukua mkondo wao wa kufundisha jamii na kuonya hasa haki ilipozuiliwa.
- Waandishi, Mafarisayo na Masadukayo kwa sehemu nao walifundisha kuhusu torati na ibada.

**Agano Jipya**

- Agano Jipya linatanguliwa na Yohana mbatizaji – alikaza toba iletayo ondoleo la dhambi
- Yesu mwenyewe – "Rabi" au mwalimu yeye alikuwa mwalimu wa pekee. Na aliwaagiza wafuasi wake kufundisha: "Enendeni ulimwenguni mwote …" Huyu alibaki kuwa mwalimu wa pekee mpaka leo – mafundisho yake yakiwa na agenda kuu ya upendo.
- Mitume na hasa mtume Paulo ni walimu wa pekee wakiyafundisha makanisa mapya huko Asia.
- Watu walioamini, walibatizwa kwanza ndipo wakaendelea kufundishwa. Hata utaratibu wa ubatizo wa watoto uwe na wadhamini ili wawatunze watoto kimafundisho ulianza baadaye.
- Wakati wa mababa wa kanisa. Kiri mbalimbali (Creeds,) ubatizo, utatu mtakatifu vilianza kufundishwa. Zamani za Giza 500 – 1500 Katekismo ambayo ilibeba mafundisho ya msingi ilitengenezwa, Luther aliboresha ya kwake tu.
- Kabla ya matengenezo Katekismo ilikuwepo. Baada ya Luther mpaka sasa kumekuwa na mitaala, mafundisho na mikazo mbalimbali kwenye makanisa mbalimbali hasa haya makubwa Roman Catholic, Protestants, Orthodoksi, nk.

**5. Walengwa wa Elimu ya Kikristo**

Tumezoea kuona Elimu ya Kikristo inahusiana na vipindi vya dini mashuleni na kwa sehemu mafundisho ya Kipaimara, Shule ya Jumapili, nk.

Tuna makundi zaidi ya kumi yanayostahili kutajwa kama walengwa wa Elimu ya Kikristo:
1. Watoto – Shule ya Jumapili na chekechea
2. Kipaimara – utafiti – ninachokumbuka:
    a. Wimbo, neno moja,
    b. Mith. 1, 7 mika 6,8, (Swali la Mission Directors)
    c. tulipeleka kuni – kwa wasiojiweza.
3. Vijana (mashuleni na sharikani)
4. Umoja wa akina mama (wanawake) – wa marika mbalimbali
a. Ibada ya wanawake na wanaume…
b. Nimeanza kusikia akina baba – Moshi mjini una umoja wa wababa – mazoezi sio kusuka
5. Ibada
    a. Jumuiya, Sala za jioni, Sala za wiki

b. Sala za asubuhi katika maeneo ya kazi.
c. Kalenda yetu…

6. Taasisi ya Familia
   a. Familia na watoto,
   b. Dini shuleni
7. Wazee na makundi mengine maalum
   a. Ibada ya wazee ilivyo muhimu kwa lugha ya kienyeji
   b. Ibada za mahospitalini
   c. Mateja kama changamoto kubwa
   d. Jambo la Mauwaji ya Albino litahitaji nguvu ya pamoja
8. Umoja wa wanafunzi katika sekondari na vyuo
9. Elimu ya Kikristo kwenye seminari zetu
10. Vyuo vya Biblia na Theologia
   a. Mchango wa vyuo vyetu kwa kazi ya kuinua Elimu ya Kikristo
   b. Tafiti juu ya mambo muhimu kama uwakili, njia za kufundishia, Mission na maadili ya kikristo

**6. Kuhubiri na Kufundisha**

Elimu ya kikristo imejikita katika mahubiri na mafundisho. Yesu anaagiza mambo yote mawili yafanyike – kuhuburi na kufundisha. Inahusu kuwafundisha wote waliojiunga na ukristo na walio nje ya Ukristo. Walio ndani tuwafundishe kuwa waishi kama imani ya Kikristo inavyowataka waishi, na walio nje tuwakaribishe na kuwahubiria habari njema za injili.

**a. Kuhuburi**
Kuhubiri kunaanza kwa kuwafanyia watu uinjilisti – maana yake ni kuwaeleza juu ya upendo wa Mungu kwao hasa wale ambao bado hawajafikiwa na habari hii njema. Kuwasaidia watu wapokee kwa shukrani:

- Zawadi ya kuumbwa, tena kuumbwa kwa sura ya Mungu.
  - Kwamba tumeumbwa kwa mfano wa Mungu ni jambo la pekee sana. Wenzetu wanaliona kama ndilo jambo kubwa na la pekee zaidi. Wanaona ile hali ya kuumbwa kwa mfano wa Mungu hakuwezi kuchezewa na hakuondolewi thamani na hadhi yake na kitu au kiumbe chochote. Ni zawadi ya pekee kwa kila binadamu. Mfano kifungu cha kwanza cha katiba ya Kijerumani (article 1) kinakaza jambo hili kwa nguvu: "Die Würde des Menschen ist unantasbar –„ the dignity of human being is untouchable."
  - Uelewa huu unafanya msingi mkubwa sana wa theologia na fikra za kimagharibi. Ndiyo maana kwa mfano wanazika watu wote bila kujali iwapo wapo kundini au la! Mtu ambaye hakuwa kundini na familia yake inataka azikwe na Mchungaji, familia inatoa fedha kiasi kadha (kwa usharika niliotumikia ilikuwa 400€) kama gharama ya mazishi. Ikishalipwa Mchungaji anakwenda kumzika. Wanaamini binadamu hawezi kuzikwa kama mnyama au kuadhibiwa siku ya msiba wake.
  - Nilipomzika mmoja bila liturgia ya ibada ya kawaida, baada ya wiki mbili nilikutana na mtu aliyeshuhudia ile shughuli akaniuliza: "Mchungaji, yule mtu mliyemzika hivihivi ubatizo wake uliishia wapi?" Alitaka kuuliza neema ya Mungu inakomea wapi?

  - Hata nadharia ya haki za binadamu -"Human Rights" ina msingi katika ufahamu huu. Binadamu yeyote anayo chapa ya Mungu isiyoguswa na mtu yeyote hata kama anaonekana kuwa na dhambi machoni petu.
- Zawadi ya kuokolewa kwa njia ya msalaba

  Kwa kumtuma Yesu kufa kwa ajili yao. Mfano wa Kifo cha Yesu. Huu ni upendo mkuu. Hakuna upendo zaidi ya mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake.
- Zawadi ya vipawa mbalimbali vya Roho Mtakatifu
  - Vipawa hivi tunaviona kila mahali. Tena vinaonekana katika dini nyingine, ishara kuwa Roho wa Mungu yupo hata nje ya Ukristo.

Watu wakihubiriwa vema juu ya zawadi au fadhili hizi kuu tatu, kuumbwa, kuokolewa na kupewa karama za rohoni wanaongoka, wanaokoka, wanaanza kuwa wafuasi wa Bwana Yesu. Ni katika hatua hii muhimu mtu huutambua utu wake kama Petro kwa kusema: "Ondoka kwangu ee Bwana, maana mimi ni mwenye dhambi…" (Lk: 5:8) na anayefikia hatua hii Yesu aweza kumwambia "katika mwamba huu nitalijenga kanisa" (Math. 16:18).

**b. Kufundisha**

Wakati kuhubiri (proclamation – kerygma) ni maelezo ya habari za wokovu kwa namna ambayo msikilizaji hategemewi kuuliza maswali (monology), Mafundisho yanajengwa kwa namna ambayo wafundishwaji wanaweza kushiriki kuliongezea somo uwezo kwa kuuliza maswali, kupanga na kuchagua mada (dialogue).

Hata hivyo zipo nguzo muhimu nne kitheologia za kufundisha kama zilivyorithiwa kutoka kwa kanisa la mwanzo. Kanisa linapaswa kujiangalia katika ufundishaji wake wa Elimu ya Kikristo kama linalenga mambo haya manne muhimu:
- Kushuhudia (**marytria**), - imani hushuhudiwa
- Ibada (**leturgia**) – Imani huonyeshwa kwa nje - kile kinachoaminiwa kwa ndani hutafutiwa muundo unaoonekana (expression of faith).
- Hudama za kijamii za kikristo (**diakonia**) – imani watu huiishi si kwa maneno tu ila pia kwa matendo.
- Ushirika (**koinonia**).

Missioni maana yake ni kushuhudia, ibada, diakonia na ushirika.

**i. Kushuhudia (marytria) – Imani hushuhudiwa**

Ni lazima kuwafundisha wafuasi wapya na wa zamani kuwa kila aliyebatizwa ni mmisionari.
- Mpaka mtu abatizwe kunakuwa na tendo la kimisionari – kwamba kuna watu wamemtembelea na kumweleza Habari Njema za Yesu - akafunguka na kupokea kipawa cha wokovu na kukubali - kuokoka.
- Ni lazima mafundisho yetu yakaze pia kuwa umisionari haukomi, ukishabatizwa na ukionja uzuri wa kipawa hicho huwezi kukaa kimya, utaanza kushuhudia, hapa kazi ya Injili huanza ndani ya mtu. Tunaona mitume na hasa Petro wakiacha kazi zao na kuanza kuhubiri Injili. Mtume Paulo ni mfano mzuri – akiwaandikia Warumi anasema "tubadilishwe nia zetu" - zielekee kujitoa zaidi kwa kazi ya Mungu (Rum 12:2).
- Hata wale ambao hawana kipawa cha kuzungumza wafundishwe kuwa wanaweza wakahubiri kwa matendo yao na maisha yao mazima, ni pamoja na sadaka zao.

- Askofu mwanamke, Prof. Margot Kessmann, ambaye alikuwa mkuu wa kanisa zima la kilutheri kule ujerumani akikaza namna hii ya umisionari bila maneno aliandika:
- “Missioni maana yake: ishi kwa namna inayovutia mpaka watu waulize kwanini unaishi hivyo – useme mimi ni mkristo”!
- Mch. Dr. Andrew Kyomo, mwalimu wetu huko Makumira (Naamini sasa ni Professor) miaka hiyo alitufundisha umuhimu wa maisha yenye ushuhuda akitumia methali kutoka Msumbiji: “Matendo yako yanapiga kelele kiasi ambacho siwezi kisikia unachofundisha”.

Matendo yetu yanazungumza kuliko mahubiri au mafundisho yetu.

**ii. Ibada (Liturgia) – Imani huonyeshwa kwa nje kuleta uhalisia**

- Watu wafundishwe vizuri kuwa ibada ni mahali pa pekee ambako Mungu anakutana na watu wake kuwasikiliza na kujadiliana nao. Ibada iheshimiwe. Ibada ni namna ya kuonyesha tunachokiamini kwa namna inayoonekana kwa macho. Ndio maana ibadani siyo mahali pa kutambulishia viongozi wa kisiasa, mambo ya ukuta au hapa kazi tu sio mahali pake. Ibada ni ibada!
- Mfumo wa ibada shirikishi, zenye kwaya, vijana kusoma masomo, maigizo, wazee kushiriki sala, nk – ni njia pekee ambayo Mungu anakutana na hawa washiriki na kuwahudumia na kwa njia yao kuwahudumia wengine. Ibada zilizoandaliwa vema huwafanya washarika wakutane na Muumba wao vizuri. Ibada iliyoandaliwa vizuri ni pamoja na Mchungaji aliyetulia.

  Mchungaji wetu wa usharika zamani alifanya mara nyingi huduma mwenywe. Hakuwa mtu shirikishi. Siku moja alipotoa sakrament ibadani alifika mahali bila kujua akachoka. Wengi wetu ni mashahidi kuwa tunao wachungaji wanaong’ang’ania mimbara yao, haiguswi, ni yeye tu na vile vimifano vyake vya kila siku.

  Na asivyoshauriwa sasa, huyu mchungaji wetu alipogawa mkate na nvinyo kwa watu kama miatano hivi, wakati fulani baada ya kutoa mvinyo, akaona watu wanasubiri, hakujua wanasubiri baraka, alidhani wanasubiri mvinyo, akawapa tena mvinyo. Ni hali ya ile ya “shikamoo Mungu”, hakuuliza, na watu kwa kumuogopa Mchungaji hawakumwambia - walipokea mvinyo kwa mara ya pili. Damu ya Yesu mtu hashibi, ni kweli. Lakini kama ilikuwa kali inaweza kuleta shida.

  Kule chuoni wakati wetu Mchungaji wa Usharika aliwahi kutuomba radhi akisema: “samahanini wapendwa, juzi haikuwa ‘strong’ maana ‘parish worker’ alisahau akazidisha maji, tutarekebisha jambo hilo wiki ijayo”. Kwa usharika wetu, baba mchungaji alishangaa, mvinyo mara mbili, wabibi wachache baada ya baraka walishindwa kurudi kwenye vitu vyao, walisikika wakitamka maneno ya ajabu ajabu na wengine walinyoosha hadi nje na wengine walikwenda nyumbani bila kutoa sadaka.

Ibada inahitaji utulivu mkubwa sana. Ibada inaweza kuwa ni ibada ya mahubiri au wakati mwingine ibada ya mafundisho.

- Wakati fulani nilifanya ibada ya wanaume peke yao na wanawake peke yao.

- Ibada ya vijana na Sunday School lazima ziandaliwe pia vema kukutana na haja za kundi husika.
- Ibada ni senta muhimu ya mafundisho ya kikristo.

**iii. Huduma za kijamii za kikristo (Diakonia)**
Watheologia ni mashahidi kuwa kuna mgongano wa kimaslahi kati ya watheologia na wadiakonia. Wakati watheologia wakijiita wahudumu muhimu wa Neno (maana roho ni muhimu kuliko mwili - mwili ni gereza la roho kulingana na falsafa za zamani), wadiakonia wamebaki wahudumu wa huo mwili, mwili ambao utabaki hapa duniani na hautaurithi uzima wa milele.

Hivyo kwa muda huduma kuu imeonekana ni huduma ya Neno. Mishahara ya wachungaji ipo juu sehemu nyingine mara mbili ya ile ya wadiakonia – nahisi sababu zinazotolewa ni hii kuwa - Wachungaji husoma zaidi.

Wala sio dayosisi nyingi zina huduma ya diakonia - au kama ipo hufanyika kwa njia nyingine. Kwa nchi nyingi, mfano Ujerumani, hali hii ya mvutano imesababisha huduma ya Diakonia ijitenge na iwe nje ya kanisa. Utume wetu unategemea huduma hizi kwa usawa – zote zina wajibu wa kujenga na kuendeleza Ufalme wa Mungu – kwa njia ya Neno na kwa njia ya huduma za kijamii.

Mchungaji na mwandishi wa vitabu vya kiswahili, Dkt. Gerson Mgaya, katika moja ya maandiko yake anatoa mfano wa mhubiri mmoja aliyekuwa anahubiri kwenye treni. Akihubiri kwenye behewa moja alishangaa mmoja wa wasikilizaji wake alikuwa akilia wakati wote. Kwa mhubiri wa Neno hilo siyo jambo baya – ina maana Injili inaingia, wanasema wenyewe "Injili inapenya sawasawa". Wahubiri wengi wamekutana na hali hii. Wahubiri wengine lazima walize watu, wana vipawa vya kuliza watu. Yesu hakuliza watu!

Mhubiri mmoja alipomuuliza mama mmoja kwa nini alikuwa analia wakati wa kipindi cha neno alijibu: "Unajua kila ukija kuhubiri nikikuangalia ndevu zako ninamkumbuka mbuzi-beberu langu lililokufa ghafla – na hapo machozi lazima yanitoke".

Huyu mwinjilisti wa kujitolea kwenye behewa la treni alipotaka kujua neno lilivyopenya kwa mtu wake alimuuliza pia kwanini alikuwa unalia akihubiri? Akajibu: "Siku moja mimi na rafiki yangu tuliwaona masista wanaochangisha fedha za kujenga kituo cha diakonia cha kutunza watoto wa mtaani. Mimi niliwachukia masista. Badala ya kuwapa pesa, niliwatemea mate. Sista mmoja alichukua kitambaa na kufuta mate yale na baada ya hapo alinitazama kwa macho ya huruma na kuniambia, "mate yalikuwa kwa ajili yangu, lakini tafadhali tupe pesa kidogo kwa ajili ya watoto wa Yesu wanaoteseka mtaani. Sikutoa sadaka yoyote. Leo nimesikia tena habari za Yesu wa wale masista, utaacha kulia?" Hatuambiwi huyu kijana aliongoka, lakini katika mfano huu, na machozi hayo, huduma ya mdiakonia (sista) ilikuwa zaidi ya huduma ya Neno ya mwinjilisti wa kujitolea kwenye behewa - ikiwa mtu atajaribiwa kuzitenganisha na kuzilinganisha huduma hizi.

**iv. Ushirika – Koinonia**
- Tunaamini kuwa imani pia husherehekewa. Hapa ni zaidi ya kushiriki pamoja mwili na damu ya Bwana wetu Yesu Kristo. Elimu ya Kikrstio inapaswa ijenge washarika na

wafuasi juu ya ushirika, kuonyesha haja ya kuhitajiana na kuwa katika hali ya amani "hamony" – "building a loving communion." Hali hii inavuka uelewa wetu wa kimadhehebu na mafundisho -"dogma" zetu. Ni mkazo wa mafundisho yanayowasaidia watu kuwaza nje kidogo ya dunia ya dhehebu lao, nje kidogo ya dini yao, nje kidogo ya kitabu chao cha dini nk.

- Katika usharika niliokuwa nafanya kazi walitakiwa kupokea tamasha la vikundi vya dini mbalimbali duniani, tena vikundi hivyo vifanyie maonyesho hayo pale madhabahuni. Mkuu wa Jimbo na Askofu walikataa lakini wakasema baraza la usharika liammue. Baraza pia liligawanyika, lakini walikubali wakisema tutavipokea, na sisi tuone na tujifunze jinsi wengine wanavyoamini. Angenda kubwa ilikuwa, hatutaki pale madhabahu yetu inajisiwe. Huu lakini ni mtazamo wa Kiyahudi sana kuwa Mungu anakaa madhabahuni, na madhabahu nyingi zimetengwa – zina patakatifu pa patakatifu.

- Miongoni mwa mikutano ya kitheologia, kimissiologia, iliyowahi kufanyika ikihusisha madhehemu karibu yote muhimu kule Marekani, ulijadili pia juu ya ufahamu wetu muhimu: "hakuna jina jingine litupasalo kuokelewa kwalo." Kwa swali hili gumu hawakutaka kutoa jibu rahisi. Haikuwa kazi rahisi, maana sentensi hii inaweka ukuta – na sisi hatujengi ukuta - tunajenga daraja –"we are bulding bridges and not walls". Ukitata kuwagawa Wachungaji hapa kitheologia utaweza. Wapo wanaoamini:
  - njia ni Yesu tu,
  - zipo njia nyingine lakini zitakazoishia kwa Yesu kabla ya kufika mbinguni,
  - wapo wanaoamini kuwa njia ni nyingi.

Walihitimisha mkutani wao wakisema: "Hatuwezi kufundisha juu ya wakovu katika mwingine zaidi ya Yesu Kristo, hata hivyo hatuwezi kumwekea Mungu mipaka katika kazi yake ya uokoaji".

Wayahudi tunaamini watakuwa na njia nyingine ya wokovu nje ya Yesu Kristo, hao tunaamini, na wengine pia tutapaswa kuamini. Upana huu wa uelewa unaonekana pia katika mafundisho ya mtheologia wa zamani, Carl Bath, anapoulizwa baada ya ibada na mama mmoja mjane.
Mjane: "Ni kweli Professor, kuwa kule mbinguni tutaonana na wapenzi wetu?
Carl Bath: "Ndio, na wengine pia". Hata wale ambao sio wenzi, sio wapenzi wetu, sio wa dini yetu. Ni katika msingi huu

Elimu ya Kikristo ina wajibu wa kuendeleza jamii yenye mshikamano, jamii inayojenga daraja, inayojali amani na haki ili kuleta utulivu na ushirika, lakini bila kupotosha ukweli wa Neno la Mungu. Waalimu wa Elimu ya Kikristo watapaswa kukumbuka kuwa dini ndizo chimbuko kuu la migogoro duniani – pamoja na mawazo kuwa dini ya kikristo inaleta amani. Hata hivyo dini hazina migongano, lakini watu, waumini.

Hii inatukumbusha sisi kama wahubiri na wafundishaji kuwa tunapaswa kuheshimu mawazo na imani za wengine. Mtazamo wetu juu ya dini nyingine lazima ubadilike. Hata hivyo, kukua ni kuacha dhana ya kupambana kubadilisha wengine, bali kupambana kujibadilisha. Juzi juzi tumekutana na maneno ya hekima ya mwalimu wa dini ya Buddha yakisema:

- Maturity is when you stop trying to change people, and instead focus on changing yourself.
- Maturity is when you accept people for who they are.
- Maturity is when you understand that everyone is right in their own perspective.
- Maturity is when you learn to "let go" – "live and let live."

**7. Changamoto katika Elimu ya Kikristo**
Elimu ya Kikristo ina changamoto nyingi. Hata hivyo tukibaki katika kichwa chetu "Mchungaji na Elimu ya Kikristo" tutaona baadhi ya mambo muhimu ya kuangalia pamoja:

**a. Hadhi ya Wafundishaji – Wachungaji**
Elimu ya Kikristo ina wafundishwaji na wafundishaji. Wafundishaji wa Elimu ya Kikristo, wawe wachungaji au watu wengine, wanategemewa kuwa watu waliokwisha badilishwa na elimu hii – "E**limu ya Kikristo ni Elimu ya Mabadiliko.**" Haina maana kufundisha habari ambazo wewe mwenyewe huziamini au hazijakubadilisha.

Mwalimu mzuri ni yule anayeweza kuonyesha pia kwa hisia zake kuwa anakiamini anachokifundisha ndipo anaweza kuwafikishia ujumbe wale wanaomsikiliza. Kuhitimu mafunzo katika chuo cha theologia hatukoshi kuwa mwalimu wa Elimu ya Kikristo? Labda kunaweza kukusaidia kuwa Mchungaji, lakini siyo Mwalimu wa Elimu ya Kikristo.

Mkuu wa chuo mmoja wa Makumira alipoulizwa na wazee mbona Wachungaji wanaohitimu wengine hali ni mbaya kabisa alijibu: "Makumira ikiletewa mbuzi mwishioni anatoka mbuzi aliyeelimika, ikiletewa kondoo anatoka kondoo aliyeelimika." Alimaanisha Makumira siyo kiwanda cha kubadilisha mbuzi kuwa kondoo. Mbuzi walioelimika siyo lazima wanaweza kuwa waalimu wa Elimu ya Kikristo. Tabia muhimu ni pamoja na:

**i. Adabu kwenye Fedha na Mahusiano ya kijinsia**
Kuna namna ya maisha ya Mchungaji inaweza kusababisha washarika wahisi wamemzidi mchungaji wao kwa kiwango cha ukristo na hata cha kawaida mambo ya kibinadamu. Mmoja juzi juzi alitoa mfano jinsi anavyomzidi Mchungaji wake, akasema: "Baba Mchungaji wetu usimwonyeshe noti, ni shida. Mimi ukinipa sadaka naifikisha kanisani, mchungaji wetu hafikishi, maana yeye eti ni kuhani, yeye ndio kanisa – anaipokea na kuila." Hata uaminifu kwenye ndoa namzidi".

Mwalimu mmoja amefundisha Wachungaji juzi kuwa sadaka ni wakati inapeelekwa madhabahuni. Ikishafika na kuombewa, ikabadilisha mwelekeo, inatoka madhabahuni, huwa inakuwa imeshageuka ghafla kuwa fedha na sio sadaka tena. Sasa inapaswa kuhesabiwa kwa utaratibu wa kifedha na kupelekwa benki kwa utaratibu wa kibenki, na kutumika kwa utaratibu wa kifedha, na kukaguliwa kwa utaratibu wa kihasibu. Ni sadaka tu itakapokuwa inaelekea madabahuni, ndio wakati huhitaji kuelewa ni kiasi gani, inafunikwa, ikitoka lazima ijulikane ni kiasi gani.

Ndio maana wengine wanasema "uchungaji ilikuwa zamani, siku hizi ni ajira tu" wakiamini sasa hakuna Wachungaji wema. Nami huwajibu nikisema, kwa hadithi zilizopo za Wachungaji wa zamani, ni wazi uchungaji ni sasa - wapo waliokuwa wanauwana, wenye visa, zamani walikuwa

wanashushana vyeo na matendo mengi ya kipagani, nasikia kuna ambao hawawezi kukaa ofisi moja pia hadi siku hizi. Tulihadithiwa juzi eti mmoja alipoona mchungji mwenzake (ambaye hawaelewani) amesali usharikani kwake na kuna ibada ya chakula cha Bwana, alipofika kwenye mstari ili naye ashirikishwe, alimrukaa na kutompa mkate – Mchungaji mwenzake aliyekuwa anashirikisha pamoja naye hakuthubutu kufanya hivyo, akampa mviyo - akapokea. Yule alipoona amemyima mkate lakini mwenzake amempa mvinyo, alimwangalia kwa hasira akamwambia "hata huo mvinyo haukusaidii" – akimaanisha yeye mtoaji umemsaidia. Kila kada ina maadili yake - "professional code of conduct." Kwa Wachungaji kuna tabia za msingi - "minimum ethical standards".

Labda fedha siyo jambo rahisi. Jambo la fedha ni changamoto kubwa hata kwenye familia za washarika wetu tunaowaongoza. Tutapaswa sisi kuwa mfano. Baba na mama wanapambana na mambo ya fedha – mapato na matumizi, nani anatumia zaidi ya mwingine. Tunajua wengine hata hufikia hatua ya kuuana. Hata hivyo, mambo ya fedha na mahusino ni tamaa zinazosogeleana – haziangushi watumishi tu, hata walei.

Mama mmoja amekwenda hospitalini kumwangalia mumewe aliyekuwa amelazwa kwa kuzidiwa. Yule mama alikuwa mzuri. Daktari alipomwangalia yule mama alivyo mzuri akashtuka. Mama naye alipomwangalia mumewe aliyeishiwa nguvu hapo kitandani alisema moyoni, kwa nini sikuolewa na daktari? Yule baba alikuwa kama ameshaishia, daktari akawaza juu ya huyu mjane mzuri. Akajikuta amemwambia yule mama; "Mpenzi wangu, nasikitika kukuarifu kuwa mumeo amefariki." Yule baba akasikia akiwa amelala pale kitandani, pamoja na maumivu akasema kwa sauti ya uchungu, "bado sijafa jamani." Mama naye alijikuta akimjibu kwa ukali: "tulia, wewe, daktari ndiye anafahamu zaidi yako".

Pamoja na uaminifu kwenye mambo ya fedha na ndoa yapo pia mambo marahisi ambayo lazima mchungaji ayashinde ili aweze kuwa mwalimu asimamaye mbele na kufundisha:

**ii. Uwezo wa kusamehe**

Washarika na waumini wanaamini Mchungaji wao anauwezo wa kusamehe kama anavyopenda yeye mwenyewe kutangaza msamaha wa dhambi. Kama Wachungaji wananyukana wenyewe kwa wenyewe au wale wanaowaongoza kwenye mambo ya kawaida na hasa yale ya vyeo basi hawawi mfano bora kwa wengine – sio waalimu wa Elimu ya Kikristo kwa matendo yao.

Wengine wana uvundo na mizigo mikubwa moyoni, sio watu huru kufundisha huruma ya Yesu. Mchungaji mmoja alipogundua kuwa amemkosea Mchungaji mwenzake alikwenda kumwomba msamaha. Lakini yule mwenzake alikataa kuzungumza naye na alimwaambia sipo tayari kukusamehe.

**iii. Ufahamu wa Haki za Binadamu**

Baadhi ya haki za binadamu haziendani na tamaduni fulani fulani. Hata kama ni tamaduni kandamizi, hupokelewa au kufundishwa na walimu wa Elimu ya Kikristo, hasa kwenye mahubiri. Itakuwa aibu kama mitaala isiyokuwa ya kidini (secular curricula) itaweka mkazo mkubwa na kutetea haki za binadamu kuliko mitaala ya Elimu ya Kikristo. Haki hizi ni pamoja na uhuru wa kujieleza kanisani, usawa wa kijinsia, haki ya kuishi, heshima ya utu wa mtu, nk. Ni elimu inayokaza ufahamu kuwa binadamu wote ni ndugu bila kujali kabila, rangi, kanda au

jinsia. Mpende jirani yako kama nafsi yako ndio kipimo. Na Bwana Yesu ametupatia kipimo kikubwa zaidi, tupendane kama yeye alivyotupenda (Yohana 13:33).

Fikria Mchungaji anajiwa na malaika usiku anamwambia aombe chochote naye atapewa. Akaamka kwa furaha, akachukua kalamu akaanza kuorodhesha, kurasa zikawa nyingi; vingine vilisomeka hivi: kuwa Mkuu wa Jimbo na baadaye Askofu, magari mazuri ya starehe na ya biashara, nyumba za kukodisha, watoto wawe madaktari na wengine marubani wa ndege. Cha ajabu hiyo listi haikuwa na ombi hata moja la usharikani, wala kitega uchumi wala watoto yatima. Akamwamsha mkewe ili amwongezee karatasi na kumkumbusha mambo muhimu. Ghafla malaika akarudi kumpa taarifa nyingine ya nyongeza ikisema, ukumbuke kila unachoandika, ujue na Mchungaji mwenzako atapewa mara mbili. Mhh! Yaani wewe umejenga kanisa, yeye Mchungaji jirani yako atajenga kanisa na kitega uchumi, yaani wewe umeweka kwenye listi chuo kikuu, jirani yako ni chuo kikuu na benki. Alijikuta hawezi kuendelea kuandika, akajikuta akirarua ile orodha yote aliyokwisha andika, mpaka kunakucha hakupata kitu kingine cha kuandika. Baadaye aliandika: “Nitoboe jicho langu la kushoto, ili na Mchungaji mwenzangu atobolewe yote mawili nk.”

Ni rahisi kuuliza kwa hasira: huyo Mchungaji ni nani? Huyo Mchungaji ni mimi - na wewe. Hata hivyo, ni lazima tumshinde huyu baba Mchungaji tukitaka tuwe walimu wa wengine. Kumpenda jirani yako kama nafsi yako ni kuweza kumpenda Mchungaji mwenzako pia. Binadamu wote ni jirani na ndugu bila kujali kabila, rangi, kanda, jinsi, nk. Kumpenda mwingine kama Yesu alivyotupenda ni kuwa tayari kuona kwamba inapobidi mwingine apate kizuri zaidi yangu.

Mtu huyu anayeitwa Adamu wa kale yupo ndani yetu kila mmoja. Ni mtu mwenye chuki, asiyetaka maendeleo ya wengine isipokuwa wewe tu, tunapaswa kupambana naye kila siku. Msharika mmoja alimfuata mchungaji wake akamwambia:
Mkristo: “Mchungaji nasikia kwenye kifua changu kama kuna roho mbili zinapingana, moja inataka kutenda mema na nyingine maovu, sijajua ipi itashinda.”
Mchungaji: “Itashinda ile inayopata malisho zaidi, hiyo usijali itashinda”.

Hata wahindi wanafundisha vizuri juu ya hili. Guru, mwalimu wa dini ya kihindi, aliwauliza wanafunzi wake: “Ni wakati gani kunakuwa kumekucha (unapoweza kutenganisha usiku na mchana): Mwanafunzi mmoja akajibu: "Ni wakati kwa mbali ataona mnyama na kutofautisha kama yule ni ng'ombe au farasi." "Kosa" Guru alisema."Ni wakati kwa mbali mtu ataona mti na aweze kutofautisha kama ni mnazi au mti wa maembe" "Kosa tena" Alijibu Guru. "Ni wakati gani sasa" waliuliza wanafunzi. Guru Alijibu: "Ni wakati mtu anapomtazama mtu mme usoni na kugundua huyu ni kaka yake, ni wakati mtu anapomtazama mtu mke usoni na kugundua kwa ndani kuwa huyu ni dada yangu, asiyeweza hivyo, kwa huyo jua liwe popote, kwake bado ni usiku".

Wahenga walisema: “Kibatari au tochi yako haitoi mwanga zaidi kwa kuzima ya jirani.”

**b. Mitaala na Uhalisia**
Katika kizazi kipya ni lazima mwalimu wa Elimu ya Kikristo, “Mchungaji na Elimu ya Kikristo”, atambue atakutana na changamoto ya maswali mapya. Maswali mengine

yatasababisha kubadilisha mtaala wetu wa Elimu ya Kikristo katika ngazi mbalimbali hadi kwenye vyuo vyetu vya theologia ili kujenga jamii endelevu.

Ikiwa kwenye Elimu ya kawaida tu mtaala huboreshwa kila baada ya miaka 3-5, ni wazi vitabu vyetu vya Shule ya Jumapili, dini shuleni na kipa imara vitapaswa kuboreshwa mara kwa mara, hata kama kuna dayosisi, kwa utafiti wangu mdogo, wanatumia vile vya zamani mpaka leo. Wakati wakijitetea kuwa wanatunza urithi wao "tutunze urithi wetu" wakisema "old is gold" iligundulika wengi wao kuwa ni wavivu wa kujifunza mambo mapya.

Haishangazi katika mazingira haya ya kukumbatia "uzamani", watoto wanatofautiana kiufuhamu. Kwa mfano, wakati watoto wa kizazi kipya wanaposoma habari ya kufufuliwa kwa Lazaro wanauliza juu ya uwezo wa Mungu wa ufufuo, wengine wanauliza "si walifurahi sana ndugu yao kufufuka? Wakati watoto wengine kwa somo hilo waliuliza kama muujiza ule ni wa kweli, wengine walisema "ohh kabla ya ufufuo huu si kulikuwa na huzuni sana?". Cha kushangaza, pamoja na umati wa wataalamu wengi wa theologia tulio nao, mpaka sasa kuna matoleo matatu tu ya vitabu vya kipaimara tangu KKKT inanze, aidha KKKT ina toleo moja tu la dini shuleni – pamoja na mambo mengi kubadilika.

Kitabu cha nyimbo "Tumwabudu Mungu Wetu" naona labda mambo siyo mabaya, kuna matoleo kadha, habari za ubora wa matoleo nahisi leo siyo siku yake. Tena kitabu cha nyimbo hapo tumejitahidi – kuna mpaka liturgia mpya ya kuzika wasiokuwa kundini au kumbariki baba mara mama anapojifungua. Lakini kuna baadhi ya nyimbo tunahitaji kuangalia kama zilitafsiriwa sahihi nk.

- Natoa wito kuwa watu fulani au vyuo viamininiwe na kupewa jukumu la kupitia mitaala yetu ya Elimu ya Kikristo katika ngazi mbalimbali na kutoa mapendekezo. Ni rahisi tu – ni kutoa scholarship moja juu ya upimaji - "Assessment" wa mitaala yetu na hapo tunapata mapendekezo ya kitaalamu.
- Hata hivyo, mitaala mipya kwa makundi maalumu kama wazee, mateja, "homosexuals", "bisexuals" "transgender" nk., itungwe mapema iwe msaada katika jukumu zima la kuelimisha.

**c. Ulimwengu unaobadilika**

- Yapo mambo mbalimbali yaliyojitokeza kwenye jamii yetu kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na utandawazi - na yanayotakiwa kuongezwa kwenye mitaala haraka. Haisaidii kuendelea kuwa na mtizamo hasi juu ya utandawazi. Kila siku kulalamika jinsi watoto wanavyoharibiwa na utandawazi. Ni kweli kuwa hatari ya utandawazi hasa kwa mambo ya familia ipo. Internet na simu ni mifano rahisi kuwa utandawazi siyo jambo rahisi. Mfano, zamani familia ilikaa kwa mviringo, na baba au mama alielezea hadithi. Runinga ilipokuja ikaondoa ule mviringo ikaweka nusu mviringo, watu wote wakiangalia runinga. Sasa simu zimeondoa hata ile nusu mviringo. Haitachukua muda mrefu tutakuwa na watoto waliojikunja maana wamejikunja kila siku kwenye simu. Waingereza wana methali isemayo: "saa isiyokuwa na majira husema kweli angalau mara moja kwa siku".

Mambo chanya ya utandawazi ni kama yafuatayo:

1. **Ushirikishawaji**:

   Ni lazima mitaala ya mafundisho ilenge kuwasaidia watu wote, wake kwa waume, wenye ulemavu, wasiojiweza, watoto, watoto yatima na wengine waweze kushiriki katika mambo yote muhimu yanayohusu mustakabali wa maisha yao. Itakuwa bahati mbaya kama kanisa ndilo litakuwa nyuma katika dhana nzima ya ushirikishwaji, demokrasia, uhuru wa kujieleza, hasa kutoruhusu makundi mbalimbali ya kijamii hasa wanawake kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuongoza ibada (sehemu nyingine hawaruhusiwi mpaka leo kufanya huduma za kichungaji, au wanaweza tu kuwa Wachungaji lakini sio wakuu wa majimbo, maaskofu nk). Ikiwa binadamu ni nusu mke na nusu mme, ni dhahiri dini zilipaswa kuwa mstari wa mbele kuonesha njia ya kujenga usawa huu.

   Kwa mtazamo wa haraka haraka, Biblia kwa bahati mbaya imetumiwa vibaya au yenyewe sio mfano mwema katika kujenga usawa katika jamii. Mfano:

   i. Idadi ya Waisrael walioingia Kaanani inatajwa wanaume 600000 tu, wanawake na watoto hawakuhesabiwa.
   ii. Hadithi ya watu waliokula mikate wakati wa Yesu ni wanaume 5000, wanawake na watoto hawakuhesabiwa.
   iii. Mwijilisti mmoja alisikia mtu mmoja akisema kuwa Sahar ni “Mama wa Imani” na akasikia mwingine akisema “Asema mama wa Majeshi”. Aliona umagharibi na chukizi la uharibifu limeingia patakatifu.

2 Mwandishi mmoja wa Kijerumani ameandika kitabu chake kiitwacho: “Joseph, es ist ein Mädchen”, “Yusufu, ni msichanaa”. Hiyo ni sauti ya Mariamu baada ya kujifungua mtoto Yesu anamweleza mumewe kuwa Yesu aliyezaliwa siyo mwanaume kama tulivyodhani, ni msichana: “Yusufu, ni msichaha”. Mwandishi huyu alitaka kutufungua macho kuhusu uelewa wetu juu ya wanaume na wanawake. Fikiria siku Yesu amezaliwa ukute kumbe ni msichana. Yusufu angesema haiwezekani, hata manabii walisema ni mwanaume, na ikiwa ni mwanamke, hata hivyo sio kosa lake Yusufu kuzaa mwanamke. Yaani wale wachungaji wa kondeni wafike pale wakute kumbe ni msichana, wangerudi kwa huzuni makondeni mwao, mamajusi nao wangerudi na tunu zao: manemane, uvumba na dhahabu zao. Hata baadhi ya wanawake ukiwauliza Mungu ni mwanaume au mwanamke wengi husema ni mwanaume – hawakumbuki Mungu aliwaumbwa kwa mfano wao na si mfano wa mwanaume na kuwa Mungu huenda akafanana na wao. Mungu ni zaidi ya mwanaume na wanawake. Mwanamke mmoja alipoulizwa na mumewe ni akina nani wanapiga kelele huko nje alijibu: **“hakuna hata mtu, ni wanawake tu.”**

3. Juzi nilipokutana na baba wa Mchungaji mmoja wa dayosisi yetu ambaye binti yake ni Mchungaji nilijikuta namsalimu kwa kujifanya namtambua kuwa yeye ni babamkwe wa Mchungaji fulani. Naye alinisahihisha, kwa kusema mimi siyo baba mkwe wa fulani, ni baba wa fulani, sasa alitaja jina la bintiye. Niligundua mfumo dume hata mimi umetawala.

   i. Ushirikishwaji ni pamoja na kushirikisha watu wote katika mambo ya uendeshaji wa Kanisa na maisha kwa ujumla. “Ukuhani wa wote waaminio” ni pamoja na kualika watu kushika ibada, kuimba, kutoa Chakula cha Bwana, nk. Kuna sharika wazee wa usharika wanagawa mkate na Mchungaji mvinyo baada ya kuvibariki. Hii ni hatua kubwa. Makundi yote ya kijamii yatapaswa kualikwa katika ujenzi

wa Kanisa na nchi kwa ujumla. Juzi tulibishana kuwa mchungaji ikiwa akishirikisha sakramenti mwenyewe bila Mchungaji mwenzake, ajilishe mwenyewe mwishoni au alishwe na mzee. Kwa namna yetu ya "shikamoo Mungu" utaweza kulishwa na mzee?

ii. Tena ni wajibu wa mafundisho yetu kama wachungaji kuwakumbusha hata wasanifu wa majengo "archtechts" (ambao wengi ni wanaume) kusanifu majengo rafiki kwa makundi yote ya kijamii, wanawake na wanaume, kwa watu wenye ulemavu, wazee, watoto nk. Juzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam walipoanzisha kampeni ya "hedhi salama" ndipo niligundua kumbe hata mfumo wa ujenzi wa mabweni, vyoo na mifumo ya maji unapaswa kuwa tofauti na rafiki kwa makundi tofauti.

iii. Elimu ya Kikristo inapaswa kuwa sauti ya makundi haya kwenye jamii yetu. Ni elimu inayotoa mwanga kuwa makundi yote, ni elimu inayoonesha uumbaji tofauti tofauti wa Mungu – "diversity in creation and not diversion in creation". Tumefundishwa kwa makosa kuamini watu wote wenye ulemavu wanapaswa kupelekwa kwa Yesu. Hata hivyo tunapiga hatua taratibu, hawaitwi tena walemavu, hawaitwi tena watu wenye ulemavu, hawaitwi tena "watu wenye mahitaji maalum", kule India wanaitwa "watu wenye vipawa maalum – (people with special talents).

iv. Ushirikishwaji unalenga pia kugawana "keki ya nchi yetu" kwa watu wote – siyo wengine wanaishi kama malaika na wengine kama mashetani. Tutahitaji kufundisha Elimu ya Kikristo kwa upana huu wa kujenga jamii inayojali usawa kwa wote.

**d. Undelevevu – Sustainability.**
Dhana nzima ya uendelevu – sustainability - ni zaidi ya kutunza mazingira na kuotesha miti. Kinyume na kanisa la mwanzo ambalo liliwaza kuwa Yesu anarudi mapema, kanisa la sasa litapaswa kuelekeza kizazi chake katika utendaji endelevu. Kipimo cha jambo lolote kwa sasa ni jinsi jambo hilo linavyochangia kuyafanya maisha ya binadamu na viumbe vingine kuwa salama na endelevu hapa hapa duniani.

Ikiwa wahubiri wanaishi vizuri hapa duniani, ni lazima na wahubiriwa waishi vizuri hapa duniani. Hii inalenga pia jinsi ya kutunza mazingira. Ni kweli kuwa hali ya usafi wa mazingira kwa ujumla sio nzuri. Takataka vijijini bado ni changamoto. Mfano, ukiendesha gari unashauriwa uanche umbali kidogo ili kusiwe na hatari ya kugongana wakati wa kusimama ghafla. Hatari hii imeongezeka maana tafiti zinaonyesha chupa za maji na takataka nyingine zinazorushwa kwa dirishani kwenye gari iliyopo mbele yako zina uwezo wa kuvunja kio cha gari na kusababisha ajali au jeraha.

Ni kanisa ndilo lina mtandao – network - ya kufikia watu wa ndani na mashambani kuleta elimu ya mazingira. Hii ni kusema, hata uzalishaji wowote ule, uwe wa mashambani au viwandani, unapaswa ulinde ustawi wa mazingira na utu wa mtu kama jambo la pekee. Elimu endelevu ni ile inayoangalia mambo yote kwa upana wake stahili.

Hii inahusu pia utumishi endelevu katika kanisa. Tunao watumishi wengi wenye picha hafifu ya utume wao. Hawa hawafurahii kufanya kazi shambani mwa Bwana wao. Mfano, watu watatu walipokutwa wakifyatua matofali ya jengo la ibada – kanisa - waliuzwa kila mmoja anafanya nini:
1. ninafyatua matofali - Nafundisha ndoa
2. ninafanya kibarua – nimepangwa hapa.
3. ninajenga kanisa – ninajenga ufamle wa Mungu

Afanyaye kazi endelevu ni ajengaye kanisa.

**e. Mawasiliano (Communication)**
Wakati umefika Kanisa kushirikiana kwa karibu na kuwasiliana. Ni wakati sasa vyombo vya mawasiliano kama “internet” na vinginevyo vitumike. “Homepage” yetu ya kanisa ikusanye vitu muhimu kama hotuba na maandiko kadhaa kama hazina ya mafundisho.

Ni wakati sasa mtu atafungua “Homepage” yetu akutane na mahubiri mbalimbali na hasa hubiri la Jumapili. Tena kuwe na kurasa ambazo ni Wachungaji tu wanaweza kuingia ili wasome mahubiri mbalimbali kuhusu somo moja liwawezeshe kuanda kwa kufundisha Jumapili. Tovuti (Website) iwasiliane na sisi zaidi, hasa kitheologia. Hotuba, mahubiri, tafiti nk ni nguvu na chachu ya Elimu yeyote ile ikiwemo na Elimu ya Kikrtisto. Kuna Dayosisi zina webpages nzuri ambazo zinakuwa rasilimali kwa wafundishaji. Mawasiliano yanasaidia kujua wapi kuna rasilimali – Mfano dayosisi ya Mashariki na Pwani ingetusaidia kupata mashamba kule Bagamoyo, nk.

**f. Kuwekeza katika Familia**

i. Ni lazima Kanisa kuweka juhudi za makusudi kujenga na kutunza familia za kikristo. Kanisa linaanzia kwenye familia. Juzi nilipata nafasi ya kusafiri kwa muda wa siku kadhaa hapa nchini na vijana wawili kutoka Marekani - California. Kwa maelezo yao, kwenye kijiji wanachotoka ndipo makao makuu ya makampuni makubwa yalipo hasa Google, Facebook, Apple, na makampuni ya computer kama Dell nk. Wao wana ulimwengu mwingine kabisa. Kwa maelezo, baba yao ni mkatoliki wa kawaida, mama ni Myahudi wa kawaida pia kidini. Swali langu lilikuwa: Wao sasa ni dhehebu gani au dini gani? Hawana dini.

   Wamebaki hivi hivi baada ya familia yao kutokuwa na mfumo wowote wa kiibada. Na hawaoni kwa nini wasome Biblia au wawe Wakristo. Wakanipa mfano wakisema: Marekani (kwa maelezo yao), upande wa kusini wakristo ni wengi zaidi kuliko kaskazini – kusini kunaitwa “Bible belt” – wale wa migodini wanafahamu “gold belt” ni sehemu yenye dhahabu nyingi. Watu wa kusini hufurahi kuitwa “Bible belt zone”. Lakini eneo la “Bible belt” – kwa maelezo yao - lina kashfa: kwenye “Bible belt” ndiko kuna chuki na dharau kubwa dhidi ya watu weusi (racism), kiwango cha mimba za utotoni ni kikubwa na hata utoaji mimba ni mkubwa. Sababu? Mambo hayo hayafundishwi kwa undani au huelezwa tu juu juu kuwa ni dhambi au hukemewa kwa ukali tu nk.

ii. Ni kama kudhani kuwa mtoto wa Kichina akizaliwa Tanzania ataweza baadaye kuzungumza Kichina. La hasha! Akizaliwa Usukumani atazungumza Kisukuma na Uzaramoni Kizaramo.

iii. Wazazi wengi kwenye nchi za magharibi wanawapeleka watoto kwenye mazoezi mapema mara mbili kwa wiki – mtu akitaka mtoto wake awe mchezaji maarufu huanza mapema kumuuanda, hata muziki – mfano Klavier, au michezo ya aina nyininge kama tenisi watoto huanza mazoezi – "training" mapema. Wanakosea kwenye imani. Hapa wao huamini jambo la imani watoto waachiwe watakuja kuamua wenyewe wakiwa watu wazima. Mambo ya muziki na mpira wanawaamulia wakiwa wadogo ili waje kuwa mastaa halafu wanashindwa kuwaamulia mambo ya imani – hawahitaji mastaa wa kiroho.

iv. Takwimu zinaonyesha kuwa Kanisa letu – KKKT - ni la pili kwa ukubwa duniani (5.6M) likifuatiwa na Kanisa la Sweden na la Ethiopia. Watu wengi wakiulizwa siri ya ukuaji ni nini wanasema ni mipango mizuri ya kushuhudia Injili - Elimu ya Kikristo. Kwa sehemu ni kweli pia. Ukweli mwingine ni huu kuwa, kwa bahati nzuri dini imekuwa sehemu ya utamaduni mkubwa kwa sasa – ukristo ni jambo la kijamii. Mtu ni mtu kwenye jamii kama una dini fulani, mkristo au muislam. Ndio maana watoto wanabatizwa pia kama njia ya kuwaingiza kwenye utamaduni huu.

Ukristo wetu mpaka sasa unaendelea kukua kwa sababu familia zina enzi utamaduni huu. Itakapokuwa si aibu tena kuwa na watoto ambao hawajabatizwa, itapokuwa si lazima kuwa kundini au kuwa mkristo, wakati ambao watu wataamua mwenyewe mambo ya imani bila msukumo wa kijamii, kwamba watoto watapaswa kuchagua wenyenye kubatizwa au la, haitakuwa rahisi - ni kama tunavyo shughudia sasa kwa nchi za magharibi.

Kijana mmoja aliyekuwa hajabatizwa aliniambia "ninawashukuru wazazi wangu sana kuwa hawakunibatiza". Anasema: "Sioni ni sahihi watu elfu wanasema kitu kinafanana kama wimbo wa taifa, mfano Sala ya Bwana au Imani ya Mitume – kila mtu si anaweza kuomba kwa maneno tofauti?" Kuna vitu tunaelewa vizuri tukiwa watoto kuliko tukiwa watu wazima. Kanisa lazima liweke nguvu kwa watoto na vijana kwa faida ya kanisa lijalo lenye nguvu.

**8. Hitimisho**

Elimu ya Kikristo ndio mhimili wa ukuaji wa Kanisa. Kanisa litachanua na kuongezeka, kama Injili itafundishwa kwa usahihi wake. Ndio sababu ni wajibu mkuu wa mchungaji kufundisha Elimu ya Kikristo, tena kufundisha kwa weledi – ina maana kuhubiri na kufundisha marika yote na makundi yote kwa ufasaha. Elimu hii kama elimu nyingine, ina mfundishaji, mfundishwaji na kile kinachofundishwa.

Hata hivyo, kufundisha ni taaluma inayomhitaji mfundishaji kujifunza zaidi ya mwanafunzi anachotaka kufundishwa, inaweza kumaanisha kufuata mtaala fulani na mwishoni kupima matokea ya kilichofundishwa – mabadiliko. Haya ni mabadiliko yanayotokea na kuonekana kwenye fikra na tabia. Ni wazi, hii ni kazi inayohitaji mtaalamu, na kwa lugha ya Elimu ya Kikristo, ni jambo linalomhitaji mtheologia na Mchungaji.

Kwa kuwa mazingira yanatofautiana kutoka sehemu moja hadi nyingine na sasa kuna mabadiliko makubwa, ni wajibu wa wafundishaji wa Elimu ya Kikristo kujinoa kila wakati, kitaaluma na kimkakati. Kwa Kanisa zima inawe kumaanisha kuendeleza tafiti mbalimbali juu ya namna bora ya kuwafikia watu. Tafiti hizi zinaweza kulenga pia mahitaji mapya kutoka kwenye makundi mapya kama mateja, wakongwe, watu wa jinsia moja au mbili (homosexual and bisexual) na wengine wanaosubiri kufikiwa na Elimu ya Kiristo.

Muziki, sanaa na elimu nafsi ya binadamu (human lerning psychology) ni maeneo yanayohitaji kuangaliwa kiutafiti yanavyoweza kuongeza kasi ya kufikia watu wengi zaidi hasa vijana. Hili ni jambo kwa hakika litakalosababisha kurekebisha mitaala ya Elimu ya Kikristo kila wakati na katika ngazi mbalimbali. Mabadiliko yanayotokea duniani yatapaswa kupimwa na kutafsiriwa yanavyoweza kuchangia kukuza Elimu ya Kikristo.

Yesu alisema: ***"Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza katika jina la Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari." (Math 28:18).***

Imetolewa na: **Mchg. Dkt. Emmanuel Kileo** Mhadhiri Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbuya Stefano Moshi aliyeongoza Somo la Biblia kuhusu **Mchungaji na Elimu ya Kikristo.**
Kwa ajili ya **Mkutano wa Wachungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT)**, Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), 24 - 29 Septemba, 2016.

**--------------**

**VITABU VYA REJEA**

Bahendwa, Lutashumululwa F: Elimu ya Kikristo, Dodoma: 1999.
Kileo, Emmanuel Kileo: Grüß Gott aus Afrika: Deutsche Mentalität aus Sicht einer tansanischen Missionar, Neuendettelsau: 2012
Groome, Thomas H.: Christian Religious Education, San Fransico: 1980.
Lee, James Michael: The Flow of Relious Instruction, Birmingham: 1973,
Miller, Randolf Crump: Education for Christian Living, Birmingham: 1957. 29